# UCHANGANUZI WA MAENDELEO YA KISEMANTIKI KATIKA SHENG: MTAZAMO WA PRAGMATIKI LEKSIKA.

**NA**

**WARAMBO JOHN PAUL**

**Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya Uzamili katika idara ya Isimu na Lugha, Chuo Kikuu cha Nairobi.**

University of NAIROBI Library

0479824 5

**IDARA YA ISIMU NA LUGHA**

**CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**©2011**

# IKIRARI

Mtahiniwa

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na wala haijawahi kutolewa popote kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamili katika chuo kikuu kingine.

Sahihi.............................................................. Tarehe 27/10/2011 ..............................................................

WARAMBO JOHN PAUL.

(Mtahiniwa)

Wasimamizi

Tasnifu hii imewasilishwa kwa madhumuni ya kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na chuo kikuu cha Nairobi kupitia idara ya Isimu na Lugha.

Sahihi.............................................. Tarehe 27/10/2011 ..............................................

Prof .John Hamu Habwe (Msimamizi)

Sahihi.............................................. Tarehe 27/10/2011 ..............................................

Dkt. Iribe Mwangi (Msimamizi)

## TABARUKU

Tasnifu hii kwanza, naitabarukia wazazi wangu; Bw. Michael Warambo na Bi. Pamela Warambo. Usaidizi wa mamangu kupitia maneno ya kunitia moyo na maombi yake yalinifaa sana wakati nilihisi kulemewa na kazi. Pili ningependa kumtabarukia kitinda mimba wetu Mildred, ambaye mama alipokuwa amebeba mimba yake sikufurahia lakini alipozaliwa aliishia kuwa rafiki yangu wa karibu sana. Mwisho tasnifu hii naitabarukia mpwa wangu Levis Otieno ambaye japo mchanga amekuwa wa kunichangamsha kwa kupiga simu na kuuliza maswali yasiyokuwa na majibu.

## SHUKRANI

Shukrani zangu ningependa kutoa kwa wale wote ambao kwa njia moja au nyingine wamechangia kukamilika kwa tasnifu hii, ama kweli hakuna binadamu ambaye ni kisiwa. Siku zote binadamu husaidia na husaidiwa.

Kwanza natoa shukrani zangu maalumu kwa wasimamizi wangu ambao maelekezo, tahakiki na maoni yao ya kitaalamu yalinifaa sana katika kazi hii; hawa ni Prof. John Habwe na Dkt. Iribe Mwangi. Pamoja na kwamba wasimamizi hawa ndio walionifungulia ulimwengu wa Kiswahili katika digrii yangu ya kwanza, pia wamekuwa walezi bora kwangu katika usomi. Hakika ahadi ya Prof. Habwe 'nitakupa usaidizi wowote utakaohitaji ukirejea katika kiwango cha uzamili' imekuja kutimia hasa alipoishia kuwa msimamizi wangu. Vikao tulivyokuwa navyo vilinipevusha zaidi. Dkt. Iribe, hadithi alizotoa kwingineko kuhusu uwezo wangu katika usomi wa Kiswahili ziliponifikia zilinihimiza kutia bidii zaidi, aidha kwa kuwa kielelezo kwangu amenikuza kiusomi. Hakika wimbo uliokuwa ukiimbwa na wenzangu` umebahatika kupata wasimamizi wazuri' ulikuwa uhalisia wa mambo.

Nawashukuru wahadhiri wote katika idara ya Isimu na Lugha, zaidi kwa wale ambao kila mihadhara yao ilikuwa nafasi ya kunitia changamoto za kuwa msomi katika uwanja huu. Shukrani maalumu kwa wahadhiri wafuatao: Prof. Abdulaziz kwa makala ya kusoma, Prof. Okoth Okombo, Prof. Wamitila, Dkt. Rayya Timammy ambaye siku zote aliamini nilikuwa mwanafunzi wake bora zaidi, Dkt. Zaja kwa kuniamini kwa mambo ya usomi, Dkt.Schroeder kwa kunihimiza na kunipa makala yaliyonisaidia katika nadharia ya kutumia, Dkt.Buregeya kwa tahakiki na makala ya kusoma, Dkt. Mbatiah ambaye usemi wake 'chema chajiuza' ulikuwa changamoto kwangu, nashukuru Dkt. Kineene kwa kuamini kwamba nilikuwa mwanafunzi wake mwenye kipawa cha usomi. Itakuwa si haki nikikosa kuwashukuru wahadhiri wafuatao ambao mchango wao katika usomi wangu hauwezi kupuuzwa: Dkt. Olali,

Dkt. J. Oduor, Dkt. Mbuthia, Dkt. Mukhwana, Bw. Amiri Swaleh. Shukrani zangu pia ziwaendee marafiki wangu kama Gilbert Omedi wa PSRI, Paul Juma wa NMG, Serah Kasembeli mwanafunzi wa uzamili katika idara ya Fasihi ya Kiingereza, Simon Mulinge, Lilian Kamulu. Zipporah Rori; mwanafunzi wa uzamili katika Kiswahili, ujumbe wangu kwake ni kwamba kama safari yangu imemalizika hata naye atamaliza. Vilevile ningependa kuwashukuru George Chanyisa kwa kuwa rafiki wa kweli, Matthias Kathuke, Evans Odhiambo, Vitus Owino, Jackson Maina na James Nyanjong. Newton Mutwiri atabakia katika kumbukumbu zangu kwa maombi yake. Fredrick Kyalo wa Safaricom namshukuru pia.

Jamaa zangu pia wamechangia pakubwa katika kuhakikisha nimekamilisha masomo yangu. Baadhi yao inanibidi kuwataja kwa majina. Nawashuruku wazazi wangu Bw. Michael Warambo na Bi. Pamela Warambo ndugu na dada zangu; Francis, George, Eunice, Henry, Peter, Antonela, Susan, Belinda, Mildreda, Vincent na Hilda. Kuna familia ambayo ningependa kuishukuru kwa kipekee sana, nayo ni familia ya Bwana na Bi Ouma Limbe, kwao nitabakia kuwa mdeni. Kwa rafiki ambaye mbali na kunifaa kwa hali na mali pia alinisaidia na tarakilishi nilipopoteza yangu Joseph Nyandemu nasema asante sana.

Katika safari hii sikuabiri peke yangu, tulikuwa na abiria wengine ambao pia nawashukuru; Lugwiri, Kamotho, Maingi Gitonga, Thamu, Wanyonyi, Mirikau, Maobe, Shitemi na Martha; mijadala tuliyokuwa nayo ilinifaidi pakubwa. Katika kikundi cha wanafunzi wa Isimu ya Kiingereza pia natoa shukrani kwa Millicent, Jane, Kibet, Sila na Kariuki. Wanafunzi wa uzamili katika programu ya masomo ya mbali natoa shukrani kwa Alex Kinyua na Bi. Mbula, imani yao kwamba nilikuwa na umahiri katika Kiswahili ilikuwa changamoto kwangu. Kwa mtangulizi wangu Veronicah Wanjiku nasema asante sana kwa makala na mashauri kwa mambo yaliyokuwa yakinisubiri. Kwa wale ambao sikuweza kuwataja kwa majina kwa sababu ya nafasi naomba wapokee shukrani zangu za dhati. Baraka !

# IKISIRI

Katika utafiti huu tulinuia kuchanganua maendeleo ya kisemantiki katika Sheng tukiongozwa na nadharia ya pragmatiki leksika ya Blutner (1990). Ili kufikia malengo hayo, sura ya kwanza imeshughulikia utangulizi kwa ujumla. Katika utangulizi tumezungumzia usuli wa mada, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, haipothesia, msingi wa kinadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada yetu, njia za utafiti na umuhimu wa utafiti huu.

Baada ya utangulizi, tulitambua kwamba leksimu ndizo hubeba maana katika lugha na hivyo kwenye sura ya pili tumezungumzia mbinu za uundaji leksimu. Mbinu zilizoshughulikiwa ni kama; ukopaji na utohozi, ubunifu, uambishaji, uambatishaji, ubadilishaji silabi, taratibu changamano, ukatizaji, onomatopea, akronimu, ujenzi ghairi, uhulutishaji, unyumbuzi kapa, ubadilishaji rajamu na upolisemia.

Leksimu baada ya kuundwa hupitia maendeleo ya kisemantiki kwa maana kwamba hubadili maana na hata leksimu kupanuka kimaana; mambo hayo yameshughulikiwa katika sura ya tatu. Hapo ndipo tumebaini mabadiliko ya kisemantiki kama njia mojawapo ya maendeleo ya kisemantiki. Aidha tumebaini michakato ya pragmatiki leksika ikiwa ni kutoa mifano ya data tuliyokusanya nyanjani.

Ili kuthibitisha hoja na madai yetu, katika sura ya nne tumeshughulikia ubunifu wa kileksimu. Ubunifu wa leksimu mpya pamoja na ubunifu wa leksimu kupata fahiwa zaidi umejadiliwa. Hapo tumetambua ubunifu wa kileksimu kama mchakato wa pragmatiki leksika huchochewa zaidi na muktadha.

Kutokana na matokeo ya uchanganuzi data, ilitubidi kurejelea haipothesia zetu ili kuzikubali. Katika sura ya tano tumetoa muhtasari wa kazi nzima pamoja na kutoa hitimisho na mwishowe kupendekeza sehemu zinazohitaji utafiti zaidi.

# YALIYOMO

Ikirari ....................................................................................................................................ii

Tabaruku ...................................................................................................................................iii

Shukrani.....................................................................................................................................iv

Ikisiri.........................................................................................................................................vi

Yaliyomo..................................................................................................................................vii

SURA YA KWANZA.....................................................................................................................1

1.0 Utangulizi...................................................................................................................................1

1.1 Usuli wa mada.............................................................................................................................1

1.2 Tatizo la utafiti.........................................................................................................................13

1.3 Madhumuni ya utafiti.................................................................................................................14

1.4 Nadharia tete.............................................................................................................................14

1.5 Sababu ya kuchagua mada...........................................................................................................15

1.6 Upeo na mipaka..........................................................................................................................16

1.7 Misingi ya kinadharia...................................................................................................................16

1.7.0 Semantiki Leksika.....................................................................................................................17

1.7.1 Pragmatiki Leksika....................................................................................................................18

1.7.1 a) Ubanifu wa kileksika...............................................................................................................18

1.7.1 b) Upanuzi wa kileksimu....19

1.7.1 b i) Kukisia maana....20

1.7.1 b ii) Upanuzi wa kikategoria....20

1.7.1 b iii) Ubunifu wa kileksimu....21

1.8 Yaliyoandikwa kuhusu mada hii....22

1.9 Njia za utafiti....28

1.9 a) Ukusanyaji data....28

1.9 b) Uchanganuzi data....28

1.9.1 Umuhimu wa utafiti huu....28

SURA YA PILI....30

2.0 Mbinu za Uundaji Leksimu....30

2.1Utangulizi....30

2.2 Ukopaji na Utohozi....31

2.3 Ukatizaji....34

2.4 Uambishaji....36

2.5 Ubunifu....37

2.6 Ubadilishaji Silabi....39

2.7 Onomatopea....40

2.8 Ujenzi ghairi.....41

2.9 Akronimu.....42

2.10 Kaleki/ Tafsiri kopa.....42

2.11 Uhulutishaji.....43

2.12 Taratibu Changamani.....44

2.13 Uambatishaji.....45

2.14 Upolisemia.....46

2.15 Unyumbuzi Kapa.....47

2.16 Ubadilishaji rajamu kuwa maneno kamili.....48

2.17 Hitimisho.....48

SURA YA TATU.....51

3.0 Maendeleo ya Kisemantiki na Ufasiri wa nadharia ya Pragmatiki Leksika.....51

3.1Utangulizi.....51

3.2 Mabadiliko ya kisemantiki.....52

3.2.1 Upanuzi.....54

3.2.2 Kubanika kisemantiki.....56

3.2.3 Matumizi ya kitamathali.....57

3.2.4 Uhamishaji wa maana.....58

3.3 Mabadiliko ya kisemantiki kama michakato ya Pragmatiki Leksika......60

3.3.1 Upanuzi wa kileksika kama mchakato wa Pragmatiki Leksika......61

3.3.1.1 Ukisivu wa kimaana......62

3.3.1.2 Tamathali kama Upanuzi wa kimaana......63

3.3.2 Muktadha kama kipengele cha Pragmatiki Leksika......65

3.4 Sababu za mabadiliko ya kisemantiki......66

3.4.1 Uboreshaji maana/ Uemeshaji maana......66

3.4.2 Udunishaji maana/ Udhalilishaji maana......67

3.4.3 Utata......67

3.4.4 Unasibu wa lugha......69

3.5 Hitimisho......69

SURA YA NNE......70

4.0 Ubunifu wa kileksimu na Ufasiri wa nadharia ya Pragmatiki Leksika......70

4.0Utangulizi......70

4.1Ubunifu wa kileksimu: Ubunifu wa leksimu mpya......70

4.2Ubunifu wa kileksimu: Leksimu kupata fahiwa zaidi......74

4.3Upolisemia......77

4.4Maoni ya wahojiwa kuhusu ubunifu wa kileksimu......78

4.5Hitimisho........................................................................................................82

SURA YA TANO........................................................................................................83

5.0 Muhtasari, Hitimisho na Mapendekezo........................................................................................................83

5.1 Utangulizi........................................................................................................83

5.2 Muhtasari........................................................................................................83

5.3 Hitimisho........................................................................................................84

5.4 Mapendekezo........................................................................................................87

Baadhi ya istilahi zilizotumika........................................................................................................88

MAREJELEO........................................................................................................91

KIAMBATISHO A........................................................................................................99

## MICHORO

Kielelezo cha 1: Semantiki leksika........................................................................................................18

Kielelezo cha 2: Ubanifu wa kileksika........................................................................................................18

Kielelezo cha 3: Upanuzi wa kileksika........................................................................................................19

Kielelezo cha 4: Ukisivu wa maana........................................................................................................20

Kielelezo cha 5: Upanuzi wa kisemantiki........................................................................................................46

Kielelezo cha 6: Upanuzi wa kimaana........................................................................................................55

Kilelezo cha 7: Nyongeza za kifahiwa........................................................................................................56

Kielelezo cha 8: Ukisivu....63

Kielelezo cha 9: Tamathali kama upanuzi....64

**JEDWALI**

Jedwali 1 : Ubunifu wa leksimu mpya....73

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Sura hii imeshughulikia utangulizi kwa jumla. Tumeshughulikia usuli wa mada–hapa tumeangazia asili ya Sheng, mielekeo, maoni, mitazamo na nadharia tete kuhusu Sheng. Aidha tumeshughulikia tatizo la utafiti na wakati huo huo tumearifu kuhusu madhumuni ya utafiti pamoja na nadharia tete. Vilevile tumetoa sababu zilizochangia uchaguzi wa mada hii. Katika sura hii vipengele vya mipaka na upeo wa utafiti vimeshughulikiwa. Yaliyoandikwa kuhusu mada hii pia tumepitia ikiwa ni pamoja na kuziorodhesha njia za utafiti huu. Mwishoni tumezungumzia umuhimu wa utafiti huu kwa jumla.

### 1.1 Usuli wa mada

Kila mara Sheng inapotajwa, hisia mseto huibuka miongoni mwa wanaisimu, wanasosholojia, wanaanthropolojia na hata waandishi wa habari. Sheng imeandikiwa maoni na wataalamu wengi tena kutoka taaluma mbalimbali. Mara nyingi badala ya maoni kutolewa kulenga Sheng maoni hayo huonekana kuvutwa upande wa taaluma za watoa maoni. Kila anayeandikia Sheng kama swala la kiisimu anapoandika, maoni yanayotolewa huwa na mapendeleo ya taaluma ya mwandishi husika. Aidha wanaisimujamii wameandikia sana Sheng lakini kwa kukita katika nadharia za isimujamii. Wanaisimu miundo ambao ni wachache waliowahi kuandikia Sheng nao huandika wakiegemea nadharia za sarufi miundo. Kwa hivyo mijadala kuhusu Sheng bado inaendelea kama ilivyo lugha yenyewe na wanafunzi wa isimu na lugha bado wanaendelea kutafitia lugha hii katika viwango mbalimbali vya usomi wao. Kumekuwepo na wataalamu wa lugha ambao hadi leo wanatatizika Sheng inapoitwa lugha. Wengi walio na mielekeo kama hii ni wanaisimu miundo ambao hupima Sheng katika mizani ya vijelezi vya lugha. Hata hivyo wanaisimujamii na wengine wenye

kuegemea sarufi amilifu wanashikilia kwamba Sheng inatekeleza majukumu muhimu ya lugha ambayo ni mawasiliano na kwa hivyo Sheng ni lugha tu. Maoni kama hayo ndiyo hata utafiti huu unachukulia kuwa yenye uzito. Kama asemavyo Widdowson (1996:71) kwamba lugha ni badilifu mno na ubadilifu huo hufanya lugha kukosa uthabiti. Muundo wa lugha husaidia tu ukiwa unaweza kuwa na thamani ya mawasiliano. Kwa sababu hiyo ubadilifu wa kimuundo hauwezi kuwa kigezo kizuri cha kutilia shaka uwezekano wa Sheng kuwa lugha. Katika utafiti huu tunaegemea sana isimu amilifu na isimu tumikizi.

Japo tunasema hivyo hatuwezi kusonga mbele na uchanganuzi wa maendeleo ya kisemantiki ya Sheng pasi na kurejelea maoni ya wataalamu mbalimbali. Hadi hapa maswali yanayotujia ni: Je, asili ya Sheng ni nini? Chimbuko lake ni wapi? Na wataalamu wana maoni gani kuhusu Sheng kwa jumla? Maswali haya yanajibiwa katika aya zifuatazo.

Sheng ni mfumo wa kiisimu ambao umekuwa telezi kwa wanaisimu pamoja na waalimu wa Kiswahili katika shule za msingi na za upili. Mazrui (1995), anasema kwamba Sheng ni msimbo wa vijana ulioanza miongoni mwa vijana wanaotoka katika jamii zenye mapato duni kiuchumi wanaoishi kwenye mitaa ya mabanda mashariki mwa jiji la Nairobi. Maoni kama haya yamewahi kutolewa na Osinde (1986), Abdulaziz na Osinde (1997). Nadharia tete hii inaendelea kusema kwamba vijana walioishi na kulala katika nyumba yenye chumba kimoja cha kulala walibuni msamiati wa siri ili wazazi wao ambao pia walilala katika chumba hicho hicho wasielewe mazungumzo yao. Kembo-Sure (1992), pia anashikilia maoni yayo hayo na kusema kuwa Sheng ni msimbo wa vijana wa rika moja. Wakati Abdulaziz na Osinde wanaposema kwamba Sheng ilianza katika miaka ya sabini, kwa upande mwingine Mazrui na Mpande (1990) na Mazrui (1995) huku akimnukuu Michael Ngugi Karanja katika *Miaka 50 katika jela* anasema kwamba huenda Sheng ilianza katika miaka ya thelathini kutokana na

mifano ya leksimu za Sheng anazotoa Karanja na kwamba lugha hii ilianza miongoni mwa wezi wa mifuko kama msimbo wao wa siri.

Spyropoulos (1987:13), naye kwa upande wake anasema kwamba Sheng ilianza katika miaka ya hamsini na kushika kasi katika miaka ya sabini. Kinachomfanya Spyropoulos kusema hivyo ni kuwa maandishi mengi katika makala ya majarida na katika magazeti kuhusu Sheng yalianza kuonekana katika miaka ya sabini. Hata hivyo hiyo haimaanishi kwamba huo ndio ulikuwa mwanzo wa lugha hii.

Kutoelewana huku kuhusu asili na chimbuko la Sheng ndiko kunamfanya Ngesa (2002) kudai kuwa hakuna asili moja ya Sheng. Ifahamike pia kwamba madai mengineyo yapo. Hata hivyo, japo hakuna mwafaka kuhusu asili na chimbuko la Sheng, mambo yafuatayo yanaweza kudondolewa:

(i) Sheng ni aina ya lugha na lugha hii inatumiwa na jamii lugha fulani kuwasiliana baina yao.

(ii) Wataalamu wengi kama vile Iribemwangi na Mukhwana (2011), Mazrui (1995), wanahusisha Sheng na vijana.

(iii) Asili ya Sheng inahusishwa na watu wenye mapato duni katika jamii na wanaishi katika mitaa inayoakisi hali hiyo. Jijini Nairobi maeneo ya kuishi watu hawa wakati unaodaiwa kuzuka kwa Sheng ni mashariki mwa jiji.

(iv) Lugha hii pia inahusishwa na uhuni na wezi wa mifuko hasa katika miaka ya kuzuka kwake.

(v) Sheng ilianzia jijini Nairobi na kisha kuenea katika maeneo mengine ya Kenya na Afrika Mashariki kwa jumla.

Kwa sababu utafiti huu haulengi kushughulikia asili na chimbuko la Sheng, madhumini hapa ni kuarifu kuhusu maswala hayo. Imekuwa vizuri kuonyesha ufahamu wetu wa mijadala tawala inayoendelea kuhusu lugha hii ambayo inazidi kuwa maarufu sana miongoni mwa vijana na kuenea kwa kasi. Katika sehemu inayofuata tunajadili misimamo, madai, maoni na nadharia tete kuhusu Sheng.

Kuna wataalamu ambao wamewahi kujaribu kutia Sheng katika makundi ya pijini na kirioli. Jambo hili hufanywa kunapohitajika kwamba lugha hii iainishwe katika kundi lake kitaipolojia. Kabla hata kuingilia kama uainishaji huo una mushkili au la, tutafafanua maana ya pijini na kirioli mtawalia.

Pijini ni msimbo amilifu uliosahilishwa ili kufaulisha mawasiliano baina ya watu wenye kuzungumza lugha tofauti za kwanza na ambao hawana lugha moja unganishi. Pijini ni lugha mchanganyiko iliyokopa kutoka lugha zilizo katika utangamano japo kuna lugha tawala katika vipengele vya kiisimu vya pijini hiyo. Lugha hiyo tawala huwa lugha msingi wa pijini hiyo kwa maana kwamba imekopa pakubwa kutoka lugha hiyo msingi. Pijini nyingi huanza katika mazingira ya biashara kama wasemavyo Trudgil (1974) na Stockwel (2002). Hivyo ili pijini iundwe huwa kuna dharura ya mawasiliano. Kwamba mahitaji ya kimsingi ya kubuniwa kwa pijini ni kutaka kufaulisha mawasiliano pale ambapo hakuna lingua franka.

Bosire (2006:185), akimnukuu Aseka (1999) anasema kwamba madai ya kuwa Sheng ni pijini yanalandana na historia ya ukoloni nchini Kenya. Bosire anasema kwamba maendeleo ya miji katika miaka ya sitini hasa kufuatia kujengwa kwa reli ya kuunganisha Kenya na Uganda kupitia Mombasa hadi Jinja yalipelekea watu wenye asili tofauti kilugha kujipata katika miji mbalimbali. Jambo hili lilipelekea kubuniwa kwa lingua franka. Hivyo msimbo

changamani ambao labda ulikuwa pijini uliundwa. Bosire anazidi kusema kwamba vipengele vya kibunifu vilionekana miongoni mwa wanajamii na vilihusu uchanganyi msimbo ambao ulizalisha Sheng. Japo si rahisi kukubali madai haya ya Bosire, ni vigumu zaidi kuyapuuzilia mbali hasa tukitilia maanani matokeo ya utafiti wa Mazrui (1995) kuhusu Sheng kama utaratibu wa ubadilishanaji msimbo.

Ni maoni yetu kwamba kutazama Sheng kama pijini ni kujitia usahali sana wa kimawazo. Mazingira ya kuzuka kwa Sheng ni mazingira tofauti sana na yale ambayo pijini zinazojulikana ziliwahi kuzukia. Vilevile vijelezi vya pijini havimudu vipengele vyote vya Sheng. Kwa maana kwamba maelezo yanayotolewa lugha za pijini hayatoshelezi kufafanua Sheng. Tunakubaliana na Osinde (1986), anaposema kwamba haiwezekani kuwa Sheng ni pijini kwa sababu maeneo yanayodaiwa kuzukia kwa Sheng yalikuwa na Kiswahili na Kiingereza ambazo ni lingua franka za maeneo hayo. Madai yayo hayo yanawiana na yale ya Mkangi (1985).

Iwapo Sheng haiwezi kuitwa pijini, swali la kuuliza ni; je, ni kirioli? Kirioli kama inavyoeleweka ni pijini iliyoimarika na kupata wazungumzaji wazawa. Kirioli huwa na upana wa kimsamiati, kisarufi na kimatumizi kuliko pijini. Katika msingi huo inakuwa vigumu zaidi kuchukulia Sheng kama kirioli kwa sababu pijini ndiyo huzaa kirioli. Labda hapa inatubidi kurejelea maoni ya Spyropoulos (1987:129), kwamba Sheng ni matokeo ya uzungumzi mbaya wa Kiingereza na Kiswahili. Spyropoulos kama Aseka, anarejelea historia ya Kenya wakati wa ukoloni. Hivyo anasema kwamba wafanyikazi katika mashamba ya wakoloni na katika miji walikuwa na uelewa finyu wa Kiswahili na Kiingereza. Kwa sababu hiyo walizungumza Kiswahili kisosanifu kilichochanganywa na Kiingereza kisosanifu. Mwishowe watoto wa

wafanyikazi hawa walichukulia mchanganyiko huu wa Kiswahili kisosanifu na Kiingereza kisosanifu na kuuzungumza kama lugha yao na hivyo Sheng ikawa ni kirioli.

Mtazamo huo wa Spyropoulos una matatizo mengi, japo katika misingi ya wafanyikazi wa mashamba ya wazungu, Sheng inaweza kuchukuliwa kuwa kirioli, kama asemavyo Bosire (2006), swala la Sheng kuwa na wazungumzaji wazawa bado ni tata sana tena telezi mno. Vilevile uchukulio kuwa Sheng imekopa asilimia kubwa ya msamiati wake kutoka lugha ya Kiswahili ni dai ambalo ni la kijumla sana. Sheng ilivyo sasa hivi imedhihirisha kuwa na lahaja nyingi ambazo zinategemea miji na mitaa ya miji. Jijini Nairobi kuna lahaja ya mashariki inayozungumzwa katika maeneo ya mashariki mwa jiji hili, vilevile kuna lahaja ya magharibi mwa jiji. Haya yote ni tukikosa kuzingatia kufululiza kwa lugha. Ni muhimu kutaja pia kwamba Sheng inayozungumzwa katika mji fulani inakuwa na misamiati mingi kutoka lugha ya asili ya mawasiliano mapana ya miji hiyo. Hivyo Sheng inayozungumzwa Kisumu inakuwa na leksimu nyingi zilizokopwa kutoka Kidholuo tofauti na Sheng ya Nyeri ambayo inaaminika kukopa kwingi kutoka Kikikuyu; maoni haya yanawiana na ya Iribemwangi na Mukhwana (2011:118) wanapozungumzia Sheng kama lugha kipindi.

Kuna wataalamu wanaotazama Sheng kama lugha msimu kama Iribemwangi & Mukhwana (2011). Lugha msimu ni lugha ambayo hukita katika msimu fulani na huaminika kutoweka baada ya msimu huo kumalizika. Lugha msimu hutumia mkakati wa kiusemi unaowatambulisha watu na kuwafanya kuhisi kuwa na umoja. Lugha msimu huwa na majukumu ya kijamii na ya kisaikolojia. Lugha msimu ina historia yake katika nchi ya Marekani hasa miongoni mwa Wamarekani weusi, Mazrui (1995:172). Weusi waliopelekwa Marekani kama watumwa na mateka waliishia kuwa huru hasa baada ya utumwa kupigwa marufuku. Aidha walibaguliwa kwa misingi ya rangi. Watu hawa walinyanyaswa na

kunyimwa haki zao. Hivyo walibuni misamiati iliyoakisi hali yao ya uduni wa kimaisha . Misamiati yenye sifa hii ilienea na pindi misamiati hiyo ilipochukuliwa na Wamarekani weupe hasa kutoka jamii zenye uwezo wa kifedha, Wamarekani weusi nao walibadili misamiati ili kuzidi kujitambulisha na kutengana na weupe wenye uwezo wa kiuchumi. Kimsingi lugha yao ilikuwa lugha msimu kwa sababu ya kubadilikabadilika kimsamiati kuandamana na msimu wa mateso yao. Hata hivyo kubadilika huku kwa msamiati hakukuashiria kubadilika kwa hali yao ya kiuchumi. Kulikuwa ni njia ya kuasi na kujitenga. Hali hiyo inapolinganishwa na Sheng, Mazrui (1995:177) anashawishika kusema kwamba Sheng ni lugha msimu inayohusishwa na vijana wanaotoka katika jamii yenye uwezo mdogo wa kiuchumi. Anazidia kusema kwamba vijana hawa ni wa kuishi katika jiji la Nairobi. Kwa sababu hiyo Sheng inakuwa lugha ya kuwatenga wenye uwezo wa kiuchumi na wale wasio na uwezo wa kiuchumi. Hata hivyo tunatofautiana na Mazrui kwa sababu hata wale walio na uwezo wa kiuchumi wana lahaja yao ya Sheng, aghalabu ndiyo lahaja inayodaiwa kuzungumzwa magharibi mwa jiji la Nairobi. Hivyo madai ya Sheng kuwa lugha msimu yanahitaji utafiti zaidi na hilo limepita mipaka ya utafiti huu.

Kuna madai kwamba Sheng inatokana na ubadilishanaji msimbo. Ubadilishanaji msimbo ni tukio la kutumia lugha mbili au zaidi katika mazungumzo au maandishi kwa kubadili neno, sentensi au kirai katika tukio la usemi-wengine husema ni uchanganyi msimbo. Mazrui (1995:176), anasema kwamba Sheng ni lugha ambayo kimsingi imekita katika ubadilishanaji msimbo baina ya lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Mazrui anasema kwamba vipengele vya Kiswahili na Kiingereza katika Sheng huishia kuchukua muundo wa kimofosintaksia wa Kiswahili. Kwa upande mwingine faridi za Kiswahili haziingii katika fremu ya kimofolojia ya lugha ya Kiingereza. Hivyo kitenzi kama *relax, come, na elapse* na vingine vingi vitachukuwa

viwakilishi kiima, njeo na hali na viwakilishi yambwa na kwa hivyo miundo ya kisheng itakuwa *alirelax , anacome, imeelapse.* Lakini hakuna kitenzi cha Kiswahili kinachochukua viambishi vya njeo na hali vya Kiingereza.

Ingawa hatuna madhumuni ya kuhalalisha yanayosemwa na Mazrui na wengine, ni muhimu kutaja kwamba Sheng ina leksimu zake ambazo hata kama zimekopwa hatuwezi kuzipuuza na kushikilia tu kuwa Sheng ni mfanyiko wa ubadilishanaji msimbo. Abdulaziz na Osinde wanatoa mfano ambao wanadai unathibitisha Sheng kama ubadilishanaji msimbo, hata hivyo katika mfano huo huo leksimu *tichee, rwanda na buu* ni leksimu za Sheng.

**Mf 1.***Woyee tichee u-si-ni-rwande buu ndi-o-i-li-ni-leit-ish-a*

Tafadhali mwalimu usinipige basi ndilo lilinichelewesha (tafsiri)

Bosire (2006:187), anasema kwamba japo ubadilishanaji msimbo ndio mfanyiko mkuu unaoendelea katika mfano 1, kuna ishara pia kwamba Sheng sio tu ubadilishanaji msimbo. Vilevile iwapo Sheng ni ubadilishanaji msimbo, basi ubadilishanaji msimbo huo utakuwa baina ya lugha nyingi sana za wenyeji wa miji. Aghalabu katika miji, watu huwa ni wa asili tofauti kilugha. Hivyo katika muktadha wa wingilugha katika miji hasa jiji la Nairobi, inakuwa vigumu sana kuchukulia kuwa kila ubadilishanaji msimbo ni Sheng. Kwa mtazamo huo kunaweza kuwa na Sheng nyingi sana kama zilivyo lugha za Kenya. Mathalani pale kunapokuwa na ubadilishanaji msimbo baina ya Kiswahili na Kiingereza ni Sheng, ubadilishanaji baina ya Kiswahili na Kikikuyu ni Sheng, udadilishanaji msimbo baina ya Kiswahili na Kidholuo ni Sheng, na kadhalika. Wakati mwingine ubadilishanaji msimbo hukumba lugha zaidi ya mbili na kuwa ubadilishanaji wenye kukumba lugha tatu.

Sheng imejumlisha leksimu kutoka lugha kadhaa. Kama anavyosema Bosire (2006), hakuna ushahidi kwamba wazungumzaji wa Sheng wana ufahamu wa lugha zote ambazo zimechangia leksimu za Sheng. Pia Sheng inadaiwa kuwa lugha ya vijana, ubadilishanaji msimbo ni tukio ambalo hujitokeza katika jinsia zote, miongoni mwa watu wenye umri wowote, na hufanyika katika maeneo mbalimbali-iwe ni maeneo ya matajiri au ya maskini. Hivyo madai ya Sheng kuwa ni tukio la ubadilishanaji msimbo ni madai yenye usahali.

Kwa upande mwingine kuna madai ya Sheng kuwa lahaja ya Kiswahili. Lahaja imewahi kufafanuliwa kama mego la lugha ambalo kiulinganishi ni ndogo zaidi kuliko lugha. Ni aina ya lugha moja, Mgullu (1999). Lahaja huwa za aina nyingi, kwa mfano kuna lahaja za kihistoria, lahaja za kimaeneo, lahaja za kijinsia na lahaja za kiumri. Lahaja za lugha moja huwa hazitingi mawasiliano baina ya watu wenye kuzungumza lugha hiyo. Sheng kwa upande wake ni tofauti. Mzungumzaji wa lugha ya Kiswahili anaweza kushindwa kufuata mazungumzo katika lugha ya Sheng. Hili linatufanya kutilia shaka uwezekano wa Sheng kuwa lahaja ya Kiswahili.

Wanaoshikilia kuwa Sheng ni lahaja ya Kiswahili wanaegemea zaidi vipengele vya kisarufi na kategoria za kisintaksia kama njeo, hali na dhamira. Vipengele hivi vinawiana katika Sheng na Kiswahili. Wapo watafiti wanaodai Sheng ni lahaja ya Kiswahili lakini wanasema ni lahaja iliyokita mijini isipokuwa miji ambayo Kiswahili kinazungumzwa kama lugha ya kwanza-miji ya pwani. Hivyo kumekuwa na uchukulio kwamba kuna Kiswahili cha pwani ambacho pia kinachukuliwa kama ndicho sanifu na kuna Kiswahili cha bara ambacho pia kimakosa kinachukuliwa kuwa ndicho Sheng.

Bosire (2006), huku akitoa mifano ya vitenzi vya silabi moja anafahamisha zaidi kuhusu uwezekano wa Sheng kuwa lahaja ya kiswahili au la. Bosire anafanya hivyo kwa kulinganisha vitenzi vya silabi moja katika miundo ya kisoukomo kama vifuatavyo:

| **Mf 2** | **Kiswahili** | **kisoukomo** |
|---|---|---|
| 2 | a) -la | ku-la |
| | b) -ja | ku-ja |
| | c) –fa | ku-fa |
| | d) –nya | ku-nya |
| | e) –cha | ku-cha |
| | f) –wa | ku-wa |

Bosire anasema kuwa katika Sheng ukanushi wa vitenzi hivi kanuni ya Kiswahili sanifu huvurugwa, kwa sababu hiyo vitenzi hivyo katika ukanushi wa kisheng vitakuwa kama vifuatavyo: **Mf. 3**

| **Sheng** | **Kiswahili sanifu.** |
|---|---|
| 3a) si-kuli | si-li |
| b) si-kuji | si-ji |
| c) si-ku-fi | si-fi |
| d) si-ku-nyi | si-nyi |
| e) si-ku-chi | si-chi |

| | |
|---|---|
| f) si-ku-wi | si-wi |

Hatukubaliani na Bosire kwamba matumizi katika mfano 3 ni Sheng. Mifano anayotoa katika mfano 3 ni matumizi ya Kiswahili kisosanifu ambacho kinaweza kuchukuliwa kama lahaja ya Kiswahili kwa mujibu wa sera na upangaji lugha. Lau kama utafiti huu ungenuia kubainisha zaidi ya hayo tungeendelea na mjadala huo. Hata hivyo hayo yako nje ya upeo wa utafiti huu.

Katika kuchangia mjadala wa Sheng kama lahaja ya Kiswahili kuna wale wanaosema kwamba mfumo wa ngeli katika Sheng ni ule tu wa Kiswahili japo Sheng imepunguza idadi ya ngeli. Maoni haya pia yanatolewa na Bosire (2006:190), anasema kuwa nomino katika ngeli ya 10 kwa mujibu wa Sheng zinawekwa katika ngeli ya 6.

| **Mf 4.** | **ngeli 9** | **ngeli 10** | **ngeli 6** |
|---|---|---|---|
| a. | mbwa | mbwa | ma-mbwa |
| b. | hewa | hewa | ma-hewa |
| c. | nguo | nguo | ma-nguo |

Kimsingi anayoyasema Bosire ni kwamba nomino katika ngeli ya 10 zinahamishwa na kupelekwa katika ngeli ya 6, ngeli ambayo kiwakilishi ngeli chake ni {ma}. Kawaida katika Kiswahili, ngeli ya 10 huwa ni nomino za ngeli ya 9 lakini katika wingi wao. Jambo kama hilo pia linakumba ngeli ya 10 na ya 11.

| **Mf 5** | **ngeli 10** | **ngeli 11** | **ngeli 6** |
|---|---|---|---|
| a. | ukame | ukame | ma-ukame |
| b. | uchawi | uchawi | ma-uchawi |

Kwa hivyo ngeli ya 10 na 11 zinafutwa kwa mujibu wa sarufi ya Sheng na nomino katika ngeli hizi huhamishwa hadi katika ngeli ya 6. Kifupi ni kuwa kuna upunguzaji wa ngeli na vipatanishi ngeli baina ya kategoria leksika katika sentensi ya Sheng. Japo tofauti za kimfumo zilizopo hapo juu zinaashiria ubainifu wa kilahaja, haiwi rahisi kusema kwa yakini kama matumizi ya viambishi vya wingi katika nomino ambazo kwa kawaida huwa hazichukui vitambulishi wingi katika Kiswahili, ni matumizi ya kilahaja. Inakuwa vigumu zaidi kuchukulia kwamba lahaja hiyo ni Sheng moja kwa moja.

Kimsingi Sheng imekopa leksimu kutoka lugha mbalimbali. Leksimu inaweza kupitia mabadiliko ya kifonolojia, kimofolojia na ya kisemantiki. Ni kutokana na uchangamani wa leksimu inayowafanya wataalamu wengi kuita Sheng lugha mchanganyiko kama walivyofanya Abdulaziz na Osinde (1997). Webb na Kembo-Sure (2000), wanasema kwamba Sheng ni lugha mchanganyiko inayozungumzwa katika miji nchini Kenya na kwamba Sheng ina sifa ya pijini na kirioli ambazo zina maana ya ujana. Wanazidi kuafikiana kwamba lugha hii inazungumzwa na wakaazi wa kisasa wa miji ambao hawana utangamano na tamaduni za kijadi za kiafrika. Abdulaziz na Osinde wanafaulisha madai ya Sheng kuwa lugha mchanganyiko wanapotoa mfano ambao wanadai kuthibitisha kwamba Sheng ni lugha mchanganyiko.

**Mf 6** : *Mababi lazima tu-wa-pig-e pasi. Kwani wanafikiri sisi hatu-demi.(Sheng)*

**7** : Matajiri lazima tuwaibie. Kwani wanafikiri sisi hatuli (tafsiri).

Neno *babi* na *dema* ni maneno mkopo lakini yamefanyiwa mabadiliko ya kisemantiki na kimofofonolojia ili kuyahawilisha. Tukichukulia mfano wa 6 kama sentensi ya Sheng na 7 kama sentensi ya Kiswahili, kuna mambo mengi ambayo yanaweza kujadiliwa zikiwemo sifa

za leksimu za Sheng. Je, Sheng ni leksimu tu au hata mfumo mzima wa sentensi unapaswa kuakisi Sheng? Hili ni suala tata na hatuwezi kulijadili katika utafiti huu. Tunachoarifu hapa ni kwamba leksimu ambazo kwa juu juu zinaweza kuchukuliwa kama maneno ya Kiswahili zinapotumika katika Sheng huwa zimekopwa na kuhawilishwa.

## 1.2 Tatizo la utafiti.

Imedhihirika katika sehemu ya usuli kuwa mijadala kuhusu Sheng imeegemea zaidi masuala ya isimujamii na kutenga vipengele vingine vya lugha hii. Wale ambao wamekita katika isimu pekee pia wamezungumzia muundo wa Sheng lakini kijumla. Miongoni mwao ni kama vile Bosire (2008,2009), Echessa (1990), Waithira (2002) na Ogechi (2005). Hivyo bado kuna pengo lililobaki hasa kuhusu semantiki ya lugha hii. Ogechi (2005), amezungumzia jinsi lugha ya Sheng inavyounda leksimu zake; amezungumzia ukopaji, ubunifu na upanuzi wa kisemantiki. Aidha Ogechi amemalizia kwa kusema kwamba ingawa watumizi lugha hii hubuni msamiati bila kunuia, ubunifu huo una mantiki fulani. Ogechi ameshughulikia vipengele vya kisemantiki vya lugha hii lakini hakuzungumzia maendeleo ya kisemantiki na mabadiliko ya kimuktadha yanayochangia ubunifu wa kileksimu au leksimu kupata nyongeza za maana au kupunguza maana. Hapo ndipo utafiti huu unapoanzia na kupiga hatua zaidi.

Tatizo la utafiti huu linahusu maendeleo ya kisemantiki yatakayobainishwa na ubunifu wa kileksimu na kuweka wazi mfumo wa kisemantiki wa maendeleo hayo hasa kutumia nadharia ya pragmatiki leksika. Katika kuziba pengo hilo, utafiti huu umeshughulikia ubunifu wa kileksimu, leksimu zilizoko katika lugha hii kupata fahiwa nyongeza au hata kupoteza sehemu za maana. Nadharia ya uchanganuzi ni pragmatiki leksika.

Utafiti huu unaongozwa na maswali haya: Je, kunayo maendeleo yoyote ya kisemantiki kupitia ubunifu wa kileksimu katika lugha ya Sheng? Je, mabadiliko ya kimuktadha

huchangia kubuniwa wa kileksimu au leksimu kupata nyongeza za maana au kupunguza maana? Je, kuna mfumo wowote wa kisemantiki unaoandamana na maendeleo hayo? Je, nadharia ya pragamatiki leksika inaweza kufafanua maendeleo ya kisemantiki katika leksimu za Sheng?

## 1.3 Madhumuni ya utafiti

Ili kujibu maswali yaliyo hapo juu, utafiti huu unaongozwa na madhumuni yafuatayo:

1. Kubainisha kuwepo kwa maendeleo ya kisemantiki kupitia ubunifu wa kileksimu katika lugha ya Sheng.
2. Kubainisha kama mabadiliko ya kimuktadha yanachangia ubunifu wa kileksimu au leksimu kupata nyongeza au upungufu wa maana.
3. Kubainisha kama kuna mfumo wowote wa kisemantiki unaoandamana na maendeleo hayo ya kisemantiki katika lugha ya Sheng.
4. Kubainisha kama nadharia ya pragmatiki leksika inaweza kufafanua maendeleo ya kisemantiki katika lugha ya Sheng.

## 1.4 Nadharia Tete

Utafiti huu unaelekezwa na nadharia tete zifuatazo:

1. Ubunifu wa kileksimu katika lugha ya Sheng unadhihirisha maendeleo ya kisemantiki.
2. Mabadiliko ya kimuktadha huchangia ubunifu wa kileksimu au leksimu kupata nyongeza au upungufu wa kimaana.

3. Maendeleo ya kisemantiki katika lugha ya Sheng yana mfumo dhahiri wa kisemantiki.
4. Nadharia ya pragmatiki leksika inatosheleza kufafanua maendeleo ya kisemantiki katika lugha ya Sheng.

### 1.5 Sababu za kuchagua mada hii

Kichocheo kikuu ni makala ya Ogechi (2005). Makala hayo ndiyo yamezungumzia semantiki ya lugha hii hasa kwa kukita katika mbinu za uundaji msamiati na taratibu za usimbaji wao. Madai yaliyomo yametupa hamasa kuchambua maendeleo ya kisemantiki ya lugha hii kwa kukita katika ubunifu wa kileksimu. Sababu nyingine iliyotuvutia kwa mada hii ni kwamba mijadala tawala kuhusu Sheng imeegemea upande mmoja tu- ule wa isimujamii.

Aidha Ogechi (2005:353), amedai kwamba watumizi lugha hii hubuni leksimu bila kunuia japo ubunifu huo una mantiki fulani, hivyo tulichagua mada hii ili kubainisha mfumo wa kisemantiki unaoandamana na maendeleo ya kisemantiki katika lugha hii.

Kama wanavyosema Iribemwangi na Mukhwana (2011:124), kwamba Sheng ni lugha ya vijana na kwa sababu idadi ya vijana inazidi kuongezeka ni lugha iliyo na mustakabali mwema ikiwa ni pamoja na kukua kwake. Kutokana na madai ya kuendelea kwa lugha hii ndipo tulichagua mada hii ili kubainisha maendeleo haya yanavyojidhihirisha kisemantiki hasa kupitia ubunifu wa kileksimu.

Pamoja na kwamba tulitaka kuonyesha upanuzi wa lugha hii, vilevile tulichagua mada hii ili kubaini namna muktadha unavyochangia maendeleo ya lugha hii ambayo inazidi kutumika na watu wengi katika jamii lugha yake hivi kwamba inakuwa tishio kwa lugha ya taifa na lugha rasmi ya nchi ya Kenya na labda utafiti huu utatoa mwanga katika sera ya kupangwa kwa lugha hii. Pia tulichagua mada hii ili kubaini mchango wa Kiswahili katika maendeleo ya

kileksimu katika lugha hii na jinsi maendeleo ya lugha hii yatakavyochangia kukua kwa Kiswahili.

## 1.6 Upeo na mipaka.

Utafiti huu unakita katika mtagusano wa semantiki na pragmatiki na jinsi mahusiko ya kimuktadha yanavyochangia ubunifu wa kileksimu na maendeleo ya kisemantiki kwa ujumla katika lugha ya Sheng. Kwa sababu leksimu za lugha hii ni nyingi mno tumekita katika maendeleo ya nomino na vitenzi. Tunashughulikia maendeleo ya kisemantiki katika Sheng, jinsi maendeleo hayo yanavyojitokeza katika ubunifu wa kileksimu au leksimu kupata nyongeza au upungufu wa maana.

Nadharia tumizi ni pragmatiki leksika kama ilivyopendekezwa na Reihard Blutner (1990). Nadharia hii ni pana mno na hivyo hatuwezi kuitumia katika vipengele vyake vyote. Tunatumia vipengele kama vile: upanuzi, matumizi ya tamathali, ubunifu wa kileksimu, ukisivu wa maana na kipengele cha muktadha. Vipengele hivi vyote vipo chini ya mchakato wa upanuzi wa maana kama anavyosema Blutner (1990).

Sheng ni lugha ambayo imeonyesha kuwepo kwa lahaja za kimaeneo, kijinsia na kiumri. Kwa sababu hiyo tutashughulikia Sheng inayozungumzwa mashariki mwa jiji la Nairobi hasa eneo la *Jeriko.*

## 1.7 Msingi wa kinadharia


Kwa sababu tunashughulikia swala la maendeleo ya kisemantiki, katika utafiti huu nadharia ya pragmatiki leksika ndiyo inayotumika. Nadharia hii iliasisiwa na Blutner Reihard (1990). Kimsingi nadharia hii imejumlisha nadharia mbili; semantiki leksika na pragmatiki. Ni nadharia iliyoasisiwa kushughulikia masuala ambayo hayakushughulikiwa katika semantiki leksika. Ifahamike kimbele kwamba Blutner (1990) kama Carston (1997,2002), Lascarides &

Copestake (1998), Sperber & Wilson (1998,2002), Wilson (2003) alifahamu kuwa muktadha ni muhimu katika uelewa wa maana za leksimu. Binadamu hutumia lugha kwa namna inavyokiuka maana za maneno zilizosimbwa katika sarufi. Wakati mwingine watu hubuni maneno mageni, wakati mwingine maneno yanatumika kwa maana mpya lakini bado mawasiliano huwepo. Aidha maneno hukopwa na kutumika kwa ukisivu tu. Kifupi maneno hutumika kwa ukiushi wa kisemantiki. Ni masuala kama haya yaliyompelekea Blutner kushughulikia mchango wa muktadha katika kuelewa maana za maneno. Uchambuzi wa kisemantiki leksika haukushughulikia umuhimu wa muktadha katika maana. Kutokana na hayo Blutner alianza kuingiza muktadha katika uchambuzi wa maana za maneno.

Hata hivyo kama tulivyokwisha dokeza, nadharia hii imechangiwa na wataalamu wengi. Blutner mwenyewe katika mwaka wa 1998 alizungumzia tena nadharia hii alipokuwa akizungumzia umbuji wa kidhana katika akili za watumizi lugha na jinsi mfanyiko huo unavyokita katika muktadha; tofauti na ilivyochukuliwa na watetezi wa nadharia ya uhusiano kwamba binadamu huwa na utambuzi wa kiakili unaomwezesha kuchagua miktadha ifaayo kutajirisha usemi. Nadharia ya pragmatiki leksika ina ukaribu sana na nadharia ya uhusiano japo msisitizo wao ni tofauti. Wakati jukumu kuu la muktadha katika uhusiano ni kuondoa utata, katika pragmatiki leksika muktadha huchangia zaidi ufasiri na ubunifu wa kileksimu.

### 1.7.0 Semantiki leksika

Katika mtazamo huu maana za maneno ni zile tu zilizosimbwa kuwasilisha dhana fulani fulani katika ulimwengu wa watumizi lugha. Lengo la semantiki leksika ni kuchunguza mahusiano ya kifahiwa ya maneno na dhana zinazowakilishwa. Kimsingi maana za maneno ni dhana na dhana hizo huwakilisha kategoria za vitu na matukio kwenye ulimwengu.




**Kielelezo cha 1. Semantiki leksika: Kutoka (PLIN 3001) 2006-07**

### 1.7.1 Pragmatiki leksika

Madai ya kimsingi ya pragmatiki leksika ni kwamba maana iliyosimbwa na leksimu inaweza kutofautiana na ile iliyowasilishwa na leksimu hiyo. Blutner (2004) kama Wilson(2003), na Wilson & Sperber (1998) anabainisha michakato miwili mikuu ya pragmatiki leksika. Nayo ni ubanifu wa kileksika na upanuzi wa kileksika (upanuzi wa kikategoria, ubunifu wa kileksimu, ukisivu wa maana na matumizi ya kitamathali.)


**a) Ubanifu wa kileksika.**

Hii ni hali ambapo neno hutumika kwa fahiwa mahsusi zaidi au kwa ufinyu kuliko ile maana iliyosimbwa na neno hilo.

**Mf 7**. *Mamodee huwasha.*

Walimu hunywa.(tafsiri)

Neno *washa* katika Sheng humaanisha vitu vingi; kunywa vileo, kuvuta sigara, kutafuna miraa na madawa mengine ya kulevya. Hata hivyo katika mfano wa 7 *washa* limetumika kumaanisha kunywa pombe na si kunywa pombe tu lakini kunywa hadi kulewa chakari. Hivyo ubanifu unafungia nje maana nyingine yoyote na kuruhusu ufasiri mmoja-ule wa kunywa pombe hadi kulewa chakari.



**Kielelezo cha 2. Ubanifu wa kileksika kutoka (PLIN 3001) 2006-07**

**b.Upanuzi wa kileksika.**

Huu ni mchakato ambapo neno linatumika kuwasilisha maana ya kijumla zaidi. Blutner (2004) huku akimnukuu Sweetner (1990) anatoa mfano wa kitenzi 'ona' ili kufafanua tofauti kati ya maana kileksika na maana kimatumizi. Blutner anasema kuwa kitenzi hicho kinaweza kumaanisha taswira ya kiakili au kumaanisha kutumia macho kutazama kitu. Kijumla, neno linaweza kutumika kwa hali ambapo maana fasiriwa ni pana zaidi kuliko maana iliyosimbwa.


**Mf 8**

*Juma anamfil Amina.*

Juma anamhisi Amina. (Tafsiri)

Neno la Sheng *fil* ni leksimu mkopo kutoka Kiingereza na uelewa wake ni ule wa fahiwa yake katika Kiingereza ya *feel* au hisi kwa Kiswahili. Lakini katika mfano 8, *fil* ina maana ambayo imepanuliwa zaidi na hivyo mfano 8 unaweza kufasiriwa kumaanisha kwamba; Juma anajitambulisha na Amina kwa hali yake.

Kwa mujibu wa Blutner (2004), mchakato wa upanuzi wa kileksika unajumlisha michakato mingineyo ambayo ni; ukisivu wa maana, upanuzi wa kikategoria, ubunifu wa kileksimu na matumizi ya kitamathali.




**Kielelezo cha 3. Upanuzi wa kileksika: Kutoka (PLIN 3001) 2006-07**

### i. Kukisia maana


Hii ni mojawapo ya aina ya upanuzi wa kileksika ambapo neno linatumika katika ufinyu wa kimaana lakini katika ufasiri, neno hilo linafasiriwa kumaanisha mambo mengi ambayo kimsingi yako nje ya maana ya neno hilo.

**Mf 9**

*Jerii kuna wadhii rwabe.*

Jeriko kuna wasafiri mia mbili (Tafsiri).

Neno *rwabe* kawaida katika Sheng humaanisha shilingi mia mbili. Hivyo neno hilo huwa halimaanishi mia mbili kitakwimu bali humaanisha shilingi mia mbili. Hivyo katika mf 9 ufasiri unaoruhusiwa ni wa kukisia tu kwamba Jeriko ambao ni mtaa una wasafiri mia mbili.




**Kielelezo cha 4: Ukisivu wa kimaana; kutoka (PLIN 3001) 2006-07**

### ii Upanuzi wa kikategoria.

Katika matumizi lugha, hali hutokea ambapo neno lililozoeleka kumaanisha kitu au tukio fulani linatumika kumaanisha vitu vingi katika kategoria fulani ya vitu. Aghalabu mfanyiko huu hupitia majina ya rajamu ya bidhaa au biashara fulani.

**Mf 10**

*Naishia kuwahi omo.*

Naenda kuchukua omo (Tafsiri).

Omo ni rajamu inayomaanisha sabuni fulani ya unga unga. Matumizi yake hata hivyo yamepanuliwa kusimamia kategoria zote za sabuni za unga unga. Mfano mzuri katika Sheng ni ule wa neno *chuo.*

**Mf 11**

*Naishia chuo.*

Naenda shuleni (Tafsiri).

Neno *chuo* ni neno mkopo kutoka Kiswahili na humaanisha shule kunakofanywa shughuli za masomo. *Chuo* katika mfano 11 lina maana iliyojumlisha shule ya msingi, shule ya upili, chuo cha anuai na chuo kikuu. Hivyo maana yake imepanuliwa kusimamia kategoria zote za shule.

**iii Ubunifu wa kileksimu.**

Hii ni hali ambapo leksimu mpya hubuniwa na watumizi lugha. Vilevile leksimu fulani ambayo imekuwepo katika lugha inaweza kupatiwa nyongeza za maana (fahiwa). Jambo hili hutokea kwa sababu ya mabadiliko ya kimuktadha yanayopelekea kubuniwa kwa dhana za kidharura kama asemavyo Fodor (1981). Hii ni hali ambayo imepitikia lugha ya Sheng kama tutakavyoona katika sura ya nne.

**Mf 12**

*Wasee wa Buru ni masonko.*

Watu wa Buruburu ni matajiri (Tafsiri).

Awali neno lililojulikana kwa maana ya tajiri lilikuwa ni *babi.* Hata hivyo vijana wa kutoka vitongojini walipoanza kujiita *mababi* neno hili lilipoteza fahiwa ya tajiri na hivyo neno jipya likabuniwa kwa maana hiyo ya tajiri ambalo ni *sonko* kwa sasa.

Katika utafiti huu tumetumia zaidi mchakato wa tatu ambao ni upanuzi wa kileksika ambao unajumlisha michakato mingineyo mitatu. Hata hivyo ikiwa ubanifu wa kileksika kama mchakato unapotusaidia kufafanua kitu fulani pia hatuupuuzi maana pia ni mojawapo wa mchakato wa pragmatiki leksika. Aidha katika ubunifu wa leksimu mpya tumezingatia zaidi

mchango wa kimuktadha katika kubuniwa kwa leksimu mpya au leksimu kupata fahiwa nyongeza.

**1.8 Yaliyoandikwa kuhusu mada hii.**

Kazi zilizowahi kuandikwa juu ya Sheng ni nyingi, hata hivyo asilimia kubwa zimeegemea isimujamii kama tulivyokwisha fahamisha mbeleni. Aidha kazi zile ambazo zinazungumzia muundo wa Sheng ni chache na zenye kugusia semantiki ya lugha hii ni chache zaidi. Hatuwezi kupuuza yaliyoandikwa juu ya Sheng hata kama hayahusiani moja kwa moja na semantiki. Hivyo tumegusia ili kuonyesha hitimisho ya wataalamu mbali mbali. Vilevile tumeziangazia kazi zilizotumia nadharia ya pragmatiki leksika kama kifaa cha uchunguzi.

Osinde (1986) akizungumzia Sheng kama lugha ya vijana amegusia vipengele vya kimuundo vya Sheng. Utafiti wake unabainisha jinsi Sheng ilivyoegemea sana muundo wa lugha ya Kiswahili katika viwango vya kifonolojia, kimofolojia na hata kisintaksia.

Abdulaziz na Osinde (1997), nao wanatazama Sheng kama msimbo mchanganyiko unaotumiwa na vijana katika miji ya Kenya. Maoni kama haya yanaungwa mkono na waandishi wengine kama Spyropoulos (1987), Kembo-Sure (1992). Mazrui (1995), anasema kwamba Sheng ni lugha msimu wa vijana na kwamba lugha hii imekita katika ubadilishanaji msimbo. Mazrui anasema kwamba katika kiwango cha kifonolojia pia ubadilishanaji msimbo huu unajidhihirisha. Mazrui anazidi kusema kwamba faridi zilizokopwa kutoka Kiswahili na Kiingereza kwa kiwango kikubwa huhifadhi sifa zao za kiasili, Mazrui (1995:175). Hata hivyo anayoyasema mtaalamu huyu yana chembechembe za ukweli lakini hayawezi

yakachukuliwa kama ukweli kamili. Kuna faridi ambazo Sheng imekopa na kuzihawilisha kwa kuzipatia sifa zingine za kifonolojia.

**Kwa mfano 13**

*Saturday* limekopwa kutoka Kiingereza na kufanyiwa marekebisho. Kwanza neno hili limefupishwa kwa kufuta baadhi ya silabi za mwisho, kisha irabu /a/ kuingizwa baada ya konsonati /t/ na kisha ile irabu /a/ ikafanywa kuwa irabu ndefu.

*Saturday* ⟶ */sat/* ⟶ */sato/* ⟶ *[sato:]*

Vilevile katika kiwango cha kisintaksia, mpangilio wa maneno katika Sheng umechukua ule mfumo wa kisintaksia wa Kiswahili. Pale ambapo mfumo wa Kiingereza unajidhihirisha huwa ni katika virai vya kitamathali. Ni jambo hili ndilo linalomfanya Mazrui kusema kwamba sifa ya lugha msimu ya Sheng inajitokeza katika kiwango cha kileksika.

Katika kiwango cha kimofolojia, Mazuri (1995:176) anasema kwamba msingi wa mofolojia ya Sheng ni ule ule wa Kiswahili. Japo hatuna utafiti wa kuegemeza kukataa kwetu au kukubali kwetu kwa madai haya, ukweli uliopo ni kwamba utafiti zaidi unahitajika ili kubaini kwa hakika mfumo wa kimofolojia wa Sheng. Mazrui kwa upande wake anaegemeza madai yake katika mofolojia ya uambishaji- kwamba viambishi vya njeo na hali vinavyotumika katika vitezi ni vile vile tu vya Kiswahili. Mazrui anatoa mfano wa vitenzi kama vile *alirelax, anacome, imeelapse* (176). Hata hivyo, na kama anavyosema Mazrui, Sheng imeanza kupata upekee wake.

Bosire (2006) huku akidai kwamba Sheng ni lugha chotara, anasema kwamba, vijana ambao ndio watumizi wa lugha hii wamejipata katika mapisi fulani na hivyo wanatafuta njia za kuasi mipangilio ya kijamii hasa mipangilio iliyowaweka wanajamii katika ngazi tofauti tofauti

kiuchumi, kihadhi na kimaeneo. Njia mojawapo ya kuasi huku ni kutumia lugha inayopinga hali hizo ili kuwa katika usawa lakini kwa kufanya hivyo vijana hawa wamejikuta kujitenga na wanajamii. Vipengele hivyo vinajitokeza kileksimu. Maoni haya ya Bosire yanakaribiana na yale ya wanaodai Sheng ni msimbo wa siri unaotumiwa na vijana kuhifadhi siri zao miongoni mwao.

Karanja (2010) anasema kwamba upekee wa Sheng upo katika uamilifu wake miongoni mwa watumizi wake. Karanja (2010:20), anazidi kusema kwamba masuala yaliyopelekea kubuniwa kwa Sheng ni yale yasiyokuwa ya kiisimu kwa sababu kulikuwa na lingua franka ambayo ingeweza kutumika miongoni mwa vijana – lingua franka hiyo ni lugha ya Kiswahili.

Karanja vilevile akirejelea leksimu anasema kwamba Sheng imekopa zaidi kutoka lugha za Kiingereza, Kiswahili na lugha nyinginezo za makabila ya Kenya kama Kikikuyu, Kidholuo na Kiluhyia. Sheng pia imekopa kutoka Kihindi, Kigujarati, na kutoka kwa watalii wanaozuru Kenya, Karanja (2010:3). Maoni kama haya pia yanashikiliwa na Samper (2002), Spyropolous (1987). Katika uundaji msamiati, Sheng imesheheni uchotara mwingi. Uundaji huu umepitikiwa na mabadiliko mengi ya kisemantiki pamoja na ubunifu wa aina yake, jambo ambalo Karanja (2010:4) anasema ndicho kiini cha uchotara wa Sheng.

Mukhwana (2008:150), anasema kwamba Sheng na Engsh ni lugha zenye umaarufu sana katika shule za Kenya. Huku akirejelea utafiti wake alioufanya Nairobi, Mombasa and Kisumu, Mukhwana anasema kwamba wazee wanaamini kuwa wazungumzaji wa lugha hizo hawawezi kujieleza kisahihi kwa Kiswahii au kwa Kiingereza. Mukhwana anazidi kusema kwamba Sheng haina kanuni za sarufi zilizo za lazima. Hivyo neno halina maana mahsusi na kwamba muhimu ni uelewano baina ya mzungumzaji na msikilizaji. Aidha kilicho muhimu katika Sheng na Engsh ni usahili wa mawasiliano. Mtalaamu huyu ambaye amekita katika isimujamii anaeleza kwamba kama ilivyo katika Engsh, Sheng ni lugha iliyokita katika

muktadha. Anachosema Mukhwana ni kwamba muktadha ni kitu muhimu sana katika kufaulisha uelewano baina ya watumizi wa lugha ya Sheng. Kwamba muktadha ukiondolewa huenda pia maana ya neno ikabadilika. Anayoyasema Mukhwana ni kweli lakini pia leksimu za Sheng zipo na maana zao ni dhahiri na hata kama hakuna muktadha wowote, watumizi lugha hii wanaweza kudondoa misamiati na maana zao mbalimbali. Hili ni jambo ambalo tumeshungulikia katika sura ya nne. Aidha madai haya yanakuwa muhimu sana katika utafiti huu kwa sababu ya kufahamu umuhimu wa muktadha-jambo ambalo ni kipengele muhimu katika pragmatiki leksika.

Mbaabu na Nzunga (2003) wanasema kwamba Sheng ni lugha ya mijini iliyo na sintaksia kama ile ya Kiswahili na fonolojia yake vilevile inafanana na ya Kiswahili. Maoni haya si tofauti sana na yale ya Webb na Kembo-Sure (2000:37), hasa wanapofananisha Sheng na pijini. Tujuavyo ni kwamba lugha moja ambayo ndiyo huwa lugha msingi hutawala muundo wa pijini. Hivyo wataalamu wengi hukubaliana kwamba Sheng imebeba sifa za kimuundo za Kiswahili.

Githinji (2006b), amepiga hatua sana katika kujadili ubadilifu wa leksimu za Sheng. Madai yake ya kwamba Sheng inabadilikabadilika hasa katika kiwango cha msamiati ni madai ya kuangaliwa kwa jicho pevu. Tunaonelea kwamba kusema kuwa msamiati fulani hautumiki tena si kigezo bora cha kudai kwamba lugha fulani ni badilifubadilifu. Kufifia au kufa kwa msamiati huenda ni hali ya kawaida ya lugha ya kudhihirisha ukuaji wake au hata uimarikaji wake jambo ambalo utafiti huu unachunguza chini ya maendeleo ya kisemantiki.

Momanyi (2009), anaelekea kulaumu Sheng katika matumizi mabaya ya Kiswahili. Kwamba Sheng imekuwa na athari kubwa sana katika kukichafua Kiswahili. Haya ni maoni ya wengi wakiwemo waandishi wa habari na walimu wa shule za upili. Swali linalotujia ni kwamba, je, Kiswahili kisosanifu ni Sheng? Jibu la swali hili haliwezi kupatikana katika utafiti huu

maanake kufanya hivyo tutaondoka katika mipaka na upeo wa kazi hii. Lakini ni jambo la kutafitiwa kwa kina sana. Maoni haya ni muhimu kwa utafiti huu ili tusizichukulie leksimu za Sheng kijuujuu.

Kazi ambayo imepiga hatua muhimu kufungua mlango wa uchambuzi wa semantiki ya Sheng ni ya Ogechi (2005). Hadi kufikia hapa ni wazi kwamba kazi nyingi zimeegemea isimujamii ya Sheng. Madai yaliyotolewa yana miegemeo katika nadharia za isimujamii. Echessa (1990), naye anazumgumzia uundaji wa maneno katika lugha ya Sheng, Kingei (2001) vilevile. Kazi hizi zimetupa mwanga sana katika utafiti huu kwa sababu ya miegemeo ya kinadharia.

Kuna waandishi na wataalamu ambao wameshughulikia lugha msingi katika kubuniwa kwa msamiati wa Sheng. Mazrui na Mphande (1990), Ogechi (2002) pamoja na Kiessling na Mous (2001), wote hawa wanaelekea kukubaliana kuwa lugha msingi ya kubuniwa kwa leksimu za Sheng ni Kiswahii. Kwamba sarufi ya Sheng kimsingi inawiana na ile ya Kiswahili.

Katika kuzungumzia utaratibu wa kuundwa kwa leksimu za Sheng, Ogechi (2005), anapiga hatua zaidi na kuangazia mchakato mzima unaohusika katika utaratibu huu kwa jumla. Ogechi ameweka mwangaza wa kuangalia leksimu za Sheng hasa anapopambanua leksimu hizi kidaikronia. Pamoja na hayo amezungumzia uhusiano wa kifahiwa kama sinonimia. Amebaini sinonimu zinazopatikana katika nomino za Sheng. Katika vitenzi vilevile amebaini kuwepo kwa hali ya polisemia. Baada ya kufanya haya yote Ogechi (2005: 353) anaishia kutoa hitimisho ambayo ni muhimu sana katika utafiti huu. Ogechi anasema kuwa japo watumizi wa Sheng hubuni msamiati (leksimu) bila kunuia, utaratibu huo una mantiki ya hali ya juu. Alipoachia Ogechi ndipo tumechukulia na kupeleka mjadala mbele. Hata hivyo lengo la utafiti huu siyo mbinu za uundaji msamiati bali kuchambua maendeleo ya kisemantiki ya Sheng katika misingi ya nadharia ya pragmatiki leksika. Jukumu kuu ni kubaini maendeleo

ya kisemantiki yanayopitikia leksimu za Sheng na kubaini mfumo unaoandamana na maendeleo hayo.

Kuna baadhi ya kazi ambazo zimetumia nadharia ya pragmatiki leksika na ambazo pia ni muhimu kwa utafiti huu. Atichi (2004) ameshughulikia upekee wa Kiingereza cha Kenya kwa kukita katika mabadiliko ya kisemantiki. Kazi hii inatoa mwanga katika kuangazia mabadiliko ya kisemantiki, hata hivyo utafiti huu unazingatia zaidi maendeleo ya kisemantiki katika leksimu za Sheng ikiwa ni ubunifu wa kileksimu na mfumo unaoandamana na maendeleo hayo.

Mweiba (2006), naye akikita katika lugha ya Kimeru ametafiti kuhusu uhusiano wa kifahiwa kwa kulinganisha uwiano wa mahusiano ya kifahiwa baina ya Kimeru na Kiingereza. Aidha lengo la Mweiba ni kujaribia madai ya kuwa uhusiano wa kifahiwa ni bia. Japo Mweiba ametumia nadharia ya pragmatiki leksika, malengo yake ni tofauti na ya utafiti huu.

Ogola (2006), anazungumzia mawasiliano ya kiisimu na jinsi miktadha ya kijamii inavyochangia uelewa wa maana. Utafiti huu hata hivyo unazingatia mchango wa muktadha katika ubunifu wa kileksimu miongoni mwa maendeleo mengine ya kisemantiki.

Kamau (2008), anashughulikia mchango wa muktadha katika kutathmini ukweli wa usemi. Utafiti wetu kwa upande mwingine unalenga maendeleo ya kisemantiki katika leksimu za Sheng. Kazi nyinginezo ambazo zimetumia nadharia ya pragmatiki leksika ni kama vile; Munga (2009), Wambugu (2010), Makokha (2010). Kazi hizi ni muhimu sana katika utafiti huu kwa sababu zinatupa mwelekeo wa kinadharia.

### 1.9 Njia za utafiti.

Katika utafiti huu tumefuata njia zifuatazo:

**a) Ukusanyaji data**

Kwa kiwango kikubwa utafiti huu umekuwa nyanjani ili kupata data msingi. Tumekwenda kwenye maktaba pia. Tumesoma vitabu na makala kutoka majarida mbalimbali ili kupata msingi bora. Aidha kamusi hasa za Kiswahili, Sheng na Kiingereza zimetufaa sana tulipotaka kujua baadhi za maana za leksimu fulani. Hata hivyo maana za leksimu zimetolewa katika hojaji na wazungumzaji lugha hii. Tumetumia hojaji na mahojiano kama njia kuu ya kukusanya data. Mahojiano hayo yamekuwa ya ana kwa ana. Tumetumia sampuli lengwa. Data tumepata kutoka kwa wakaazi wa mtaa wa Jeriko jijini Nairobi. Tumetumia sampuli ya watu thelathini; idadi hiyo imejumlisha wanawake na wanaume. Umri wao umekuwa miaka mbalimbali.

**b) Uchanganuzi wa data**

Baada ya kukusanya data tumeichanganua data kwa misingi ya nadharia ya pragmatiki leksika. Kulipohitajika jedwali ili kufafanua hoja zaidi pia tumefanya hivyo. Kufanya hivyo kumetusaidia kuzikubali haipothesia tulizobuni. Tumechanganua data yetu huku tukitoa mifano maridhawa kuthibitisha madai yetu.

### 1.9. 1 Umuhimu wa utafiti huu

Utafiti huu umepeleka mbele uchanganuzi wa Sheng katika misingi ya kisemantiki. Aidha utafiti huu umeonyesha kwamba mbali na kuzungumzia Sheng katika vipengele vyake vya kisemantiki hasa maendeleo katika leksimu pia tumepiga hatua katika kazi hii na kubaini mfumo wa kisemantiki unaoandamana na maendeleo hayo ya kisemantiki katika leksimu za

Sheng. Aidha lugha ya Sheng inaaminika kukua kwa kasi, utafiti huu umetoa mwanga kama kweli kukua huko kunaweza kujitokeza katika kiwango cha kisemantiki kupitia ubunifu wa kileksimu.

Katika katiba mpya (2010), lugha ya Kiswahili ni lugha rasmi na lugha ya taifa vilevile. Sheng imekuwa ikishtumiwa kuchangia uharibifu wa Kiswahili. Utafiti huu utakuwa kirejelewa iwapo Sheng kama lugha ya vijana itawekewa sera mwafaka ya upangaji ili iwe na mfumo wake tofauti na ule wa Kiswahili.

## SURA YA PILI

## 2.0 MBINU ZA UUNDAJI LEKSIMU

### 2.1 Utangulizi

Katika sura hii tumeshughulikia mbinu za kuunda leksimu. Kwa kiasi kikubwa tumezijadili mbinu hizi kama mbinu bia. Kwamba ni michakato ya kilimwengu ambayo kwayo lugha yoyote huweza kuitumia ama yote au baadhi kujiundia leksimu zake. Hata hivyo tumetoa mifano zaidi ya Kiswahili na Sheng pale ambapo mifano hiyo inaafiki kufafanua au kuweka wazi maelezo. Kwa sababu mbinu hizi zina ubia, itokeavyo kuwa tumehitajika kutoa mifano ya Kiingereza au Kiswahili, vilevile tumefanya hivyo. Utafiti huu unashughulikia maendeleo ya kisemantiki kama inavyojitokeza kupitia ubunifu wa kileksimu. Baadhi ya mbinu zilizozungumziwa katika sura hii ndizo hutumika katika ubunifu wa kileksimu hasa ubunifu wa leksimu mpya katika lugha ya Sheng.

Lugha zote ulimwenguni hufikia hali ya kutaka kujiundia leksimu. Jambo hili hutokea pale ambapo kuna dhana fulani ambayo imejitokeza katika mazingira ya watumizi lugha na hakuna leksimu ya kutajia kitu hicho. Wakati mwingine lugha huunda leksimu mpya kutokana na hali ya lugha kutaka kujibadilisha ndani kwa ndani, mathalani leksimu fulani inapoanza kutumika kama neno la matusi watumizi lugha huunda leksimu nyingine mwafaka. Leksimu ya Sheng *rasa* sasa hivi inatumika kama neno matusi na hivyo watumizi lugha hii wamebuni leksimu *wezere* kama kibadala chake. Lugha kupitia watumizi wake hutumia taratibu fulani fulani ili kupata leksimu itakayowasilisha dhana mbalimbali.

Ifahamike kimbele kwamba dhana "uundaji leksimu" inatumika hapa kama istilahi ya kitaalamu. Hii ni kwa sababu uundaji leksimu katika etimolojia yake na kadri lilivyotumika

katika awamu na mapisi ya kihistoria imeonekana kukosa mpaka dhahiri wa matumizi. Wakati mwingine uundaji leksimu hutumika kwa maana ya michakato yote inayohusika katika kubadili umbo la neno kwa mfano kupitia uambishaji- jukumu ambalo ni la kimofolojia. Vilevile kwa upana wake uundaji leksimu humaanisha michakato ya kubuni leksimu mpya kama anavyochukulia,Yule (1985).

Ingawaje tofauti baina ya mabadiliko ya kimofolojia ya neno na ubunifu wa leksimu mpya ni rahisi kuelewa, bado kuna utata kama uhulutishaji uchukuliwe kama badiliko la kimofolojia au ubunifu wa leksimu mpya. Hata hivyo kuna michakato mingi ya kuunda leksimu ambayo haina utata na hivyo haijapata maoni mengi ya kukanganya. Kama anavyosema Katie 2001:269) kwamba ubunifu wa kileksimu hujitokeza kupitia michakato ya uundaji leksimu, katika sehemu ifuatayo tumezungumzia michakato hiyo na kutoa mifano ya leksimu zilizoundwa.

## 2.2 Ukopaji na utohozi

Lugha kama alivyo binadamu ina uhai. Kwa sababu hiyo lugha huzaliwa, hukua na vilevile hufa. Kuongezeka kwa leksimu na watumizi lugha huashiria ukuaji wake na kupunguka kwa leksimu na watumizi lugha huashiria kufa kwa lugha. Ni mfanyiko kama huo ambao unapitikia lugha ya Sheng. Kukua kwa lugha ya Sheng kwa kiasi kikubwa kumechangiwa na kujiundia leksimu kupitia ukopaji na utohozi.

Lugha na watumizi lugha hutangamana na lugha nyingine na watumizi lugha wengine. Utangamano huu hujitokeza na uchangamano fulani wa kiisimu. Hata hivyo kiwango cha utangamano huweza kutofautiana. Inaweza ikawa utangamano umekita miongoni mwa

watumizi lugha ikawa utangamano wa lugha zungumzi au utangamano katika lugha andishi. Matokeo ya kiisimu ya utangamano wa kilugha ni ukopaji. Ukopaji kama wasemavyo Hock na Joseph (1996:28), ni uhamishaji wa leksimu mahsusi au seti ya leksimu au faridi fulani kutoka lugha moja au lahaja moja hadi nyingine. Pale ambapo leksimu imehamishwa bila kufanyiwa mabadiliko yoyote ya kifonolojia, kimofolojia au kisemantiki huo huwa ni ukopaji sisisi. Katika upande mwingine uhawilishaji ukiandamana na ukopaji, ukopaji huo huitwa ukopaji na utohozi. Utohozi hutokea pale ambapo leksimu imekopwa kisha kufanyiwa marekebisho ya kifonolojia, kimofolojia au hata kisemantiki ili ifuate kanuni za muundo wa lugha kopeshi, Iribemwangi na Mukhwana (2011: 157). Matthews (1997:7), naye anasema kuwa leksimu mkopo zinapobadilishwa ili kuakisi mfumo wa kisauti wa lugha kopa ndipo uhawilishaji hutokea.

Kijumla baada ya ukopaji leksimu, leksimu kopwa hupatiwa uasilia wa lugha kopa. Ni katika kupokea uasilia wa lugha kopa ndipo uhawilishaji hufanywa. Lugha chagizi nayo huwa haipotezi leksimu hiyo, Arlotto (1972:184). Lakini ikitokea kwamba leksimu hiyo imepotea katika lugha chagizi jambo hilo huwa ni sadfa tu. Hivyo kupotea kwa leksimu katika lugha chagizi hakutokani na lugha kopa au hakutokani na kukopa huko. Hata hivyo Hartmann na Stork (1972:29), wanasema kuwa wakati mwingine leksimu mkopo huhifadhi sifa zake za kifonetiki na wakati mwingine leksimu mkopo huhawilishwa. Kimsingi uhawilishaji siyo kanuni ya lazima katika ukopaji leksimu.

Lugha zote ulimwenguni hukopa msamiati kama wasemavyo Fromkin na Rodman (1988:309). Kwa sababu hiyo leksikoni hujumlisha leksimu asilia na leksimu mkopo. Lugha

ya Kiingereza kama wasemavyo Hock na Joseph (1996), imekopa sana kiasi cha kufanya baadhi ya wanaisimu kudai ukopaji mwingi umefanya Kiingereza kupoteza sifa zake za kiasili. Ukopaji ni taratibu ambayo imetajirisha sana Kiswahili na hata lugha ya Sheng ambayo ndiyo tunaangazia maendeleo yake ya kisemantiki. Sheng imekopa msamiati kutoka lugha nyingi za makabila ya Kenya na hata kutoka Kiingereza, Kifaransa na lugha nyinginezo za kilimwengu. Ifuatayo ni mifano ya leksimu zilizokopwa kutoka lugha mbalimbali; baadhi ya leksimu zimehawilishwa na nyingine ni matokeo ya ukopaji sisisi. **Mfano 14**

| **leksimu mkopo** | **leksimu asilia** | **maana** | **lugha chagizi** |
|---|---|---|---|
| *mwasi* | mwasi | msichana | Kilingala |
| *buda* | budha | baba | Kigujarati |
| *wadhii* | athii | wasafiri | Kikikuyu |
| *ngiri* | ngiri | shilingi elfu moja | Kikikuyu |
| *nyoora* | sinyoora | kukojoa | Kikisii |
| *atoti* | atoti | msichana | Kidholuo |
| *dishi* | dish | chakula | Kiingereza |
| *wodee* | water | maji | Kiingereza |
| *saikoro* | msakhulu | mzee | Kiluhya |
| *katia* | kata | tongoza | Kiswahili |
| *demu* | ma'dame | msichana | Kifaransa |

Kutokana na mfano 14, kinachojitokeza ni kwamba kuna pale ambapo ukopaji sisisi hutokea, na pia kuna ukopaji na utohozi mtawalia. Leksimu ambazo zimekopwa bila kurekebishwa kifonolojia au kimofolojia hupata upanuzi wa kisemantiki; mifano ni kama leksimu; *wadhii, atoti, hanya* na *katia.* Vilevile etimolojia ya baadhi ya leksimu za Sheng kama *dishi* na *buda* inadhihirisha ukopaji wa zaidi ya lugha moja- kwa maana kwamba leksimu huweza kukopwa kutoka Kiswahili lakini leksimu hiyo ina asili yake katika lugha nyingine ingawa katika utohozi wake imepitia Kiswahili.

## 2.3 Ukatizaji

Yule (1985:54), anasema kuwa ukatizaji hutokea pale ambapo neno lenye zaidi ya silabi moja hupunguzwa silabi ili neno hilo liwe fupi kimaumbo. Iribemwangi na Mukhwana (2011:166), pia wanasema kwamba mbinu hii huhusu kufupisha majina, maneno au vifungu vya maneno. Katika mchakato huu taratibu kuu ni kufupisha silabi fulani za mwanzo, kati au za mwisho wa neno ili kujitokeza na leksimu mpya. Mbinu hii inatumika na lugha nyingine, mathalani lugha ya Kiingereza imeunda neno *fan* (shabiki) kutokana na neno *fantastic* (enye uzuri), *prof* (mtaalamu wa jambo fulani), kutokana na neno *professor* (mtaalamu wa jambo fulani). Nacho Kiswahili kina leksimu kama vile bi, ambayo ni kutokana na neno bibi, Swahili kutokana na Kiswahili miongoni mwa mengine. Ukatizaji haufungi watumizi lugha kukata silabi za mwanzo tu au za mwisho tu. Kwa sababu hiyo kuna hali ambapo Sheng inakata silabi za mwanzo kama katika leksimu *nyoora* (kukujoa) ambayo ni matokeo ya ukatizaji wa leksimu *sinyoora* pia silabi za mwisho hukatwa kama katika leksimu *doo* (pesa) kutoka *dough* (Kiingereza). Ifahamike kuwa kama asemavyo Huddleton (2002:1634), kuna aina tatu za ukatizaji; ule wa mwanzoni, mwishoni na wa kati. Imetokea kwamba Sheng inapendelea ukatizaji wa mwanzoni na mwishoni mwa neno (tazama mifano 15).

Katika Sheng, kuna leksimu zilizoundwa kutokana na ukatizaji. Hata hivyo, kabla ya ukatizaji neno hukopwa kisha linatoholewa ili kupata muundo wa lugha za kibantu na mwishowe kukatwa.Vilevile baada ya kukatwa kuna mfumo wa kurefusha silabi ya mwisho ambayo mara nyingi ni irabu. Katika mifano ifuatayo tumetumia alama za kifonetiki za kimataifa ili kuweka wazi mabadiliko ya kifonolojia yanayotokea. **Mifano 15**

| **leksimu (chagizi)** | **urekebishaji** | **ukatizaji(Sheng)** | **maana** |
|---|---|---|---|
| Saturday | sato | */sat**o**:/* | Jumamosi |
| practice | praktizi | */tizi/* | mazoezi |
| father | fadha | */fa**ð**ε**:**/* | baba |
| mother | madha | */ma**ð**ε**:**/* | mama |
| teacher | ticha | */ti**t**'ʃε:/* | mwalimu |
| dirisha | dirisha | */dir**o**:/* | dirisha |
| socket | soketi | */s**o**:/* | mia |
| kimanzi | manzi | */manzi/* | msichana |
| zamani | zamani | */zam**o**:/* | zamani |
| business | bisinesi | */bisna/* | biashara |
| hospital | hospitali | */h**o**si:/* | hospitali |
| sinyoora | sinyoora | */ɲo:ra/* | kukojoa |

Kutokana na mifano hiyo, pale ambapo ukatizaji unatokea mwanzoni mwa neno, silabi ya mwisho huwa haifanywi kuwa ndefu kwa mfano; kimanzi - */manzi/* (msichana), praktizi - /tizi/, *sɿɽo:ra- ɽo:ra* (kukojoa) -tofauti na *Saturday- /sato:/* (Jumamosi), *father- /faðɛ:/* (baba). Huu ni mfumo ambao umependelewa sana na lugha ya Sheng kutokana na iktisadi ya lugha. Vilevile jambo lingine ambalo hujitokeza katika ukatizaji wa leksimu katika lugha ya Sheng ni kwamba baada ya ukatizaji kuna baadhi ya leksimu ambazo irabu ya mwisho hubadilishwa. Mathalani; dirisha – */diro:/* (dirisha), teacher – */titʃɛ:/* (mwalimu). Bado haifahamiki kiwazi kuwa mfumo huo unachochewa na nini lakini kuna ushawishi kuhusisha mfumo huo na usahilishaji wa sarufi ya lugha.

## 2.4 Uambishaji

Katika utafiti huu, neno uambishaji linatumika kwa maana ya taratibu za kuongeza viambishi katika mzizi wa leksimu ili kuunda leksimu mpya. Matthews (1997:7) anasema kuwa uambishaji ni taratibu ya kuongeza herufi au sauti au makundi yao katika mzizi wa neno na kwamba nyongeza hiyo hubadili maana au uamilifu wa neno hilo. Maelezo haya ya Matthews ni muhimu, lakini tungependa kuongeza kwamba habari zinazobadili maana ya neno ni habari za kisarufi. Richards et al (1985), pia wanasema kuwa uambishaji ni uongezaji viambishi katika mzizi wa neno kwa madhumuni ya kuunda neno jipya. Mbinu hii inapotumika katika Kiingereza huwa kunaongezwa viambishi awali au viambishi tamati ili kupata neno jipya. Katika Sheng, mbinu hii hutumika ili kuzalisha leksimu mpya kama ilivyo katika lugha nyinginezo. Leksimu hukopwa kwanza kisha kutoholewa na baadaye kuambishwa. Viambishi pendwa katika Sheng kwa mujibu wa mbinu hii ni vile vya awali na mzizi wa neno ndio unaoambishwa.

| Mifano 16 | | | Sheng | Kiswahili |
|---|---|---|---|---|
| m | + | supa | - *msupa* | msichana |
| m | + | shii | - *mshii* | msichana |
| m | + | ngoso | - *mngoso* | mzungu |
| m | + | renga | - *mrenga* | gari |
| m | + | dosi | - *mdosi* | tajiri |

Data hii inaonyesha matumizi mapana ya viambishi awali, aghalabu katika Sheng hakuna matumizi ya viambishi kati kwa mujibu wa sarufi yake ilivyo sasa.

## 2.5 Ubunifu

Ubunifu kwa mujibu wa Hartmann na Stork (1972:29) ni mchakato au matokeo ya kuunda leksimu mpya kimaksudi kutokana na faridi za kimofolojia zilizopo. Kuna hali ambapo watumizi lugha hujitokeza na leksimu ambayo ni mpya kabisa. Kwa maana kwamba leksimu hiyo haiwezi kuhusishwa na leksimu mkopo au leksimu zilizoko katika lugha husika. Hata hivyo watumizi lugha hubuni leksimu kutokana na rasilimali walizonazo katika lugha yao. Hii ni mbinu ambayo hutajirisha lugha ndani kwa ndani. Lugha ya Sheng ni lugha ambayo pamoja na kutumia mbinu nyinginezo kuunda leksimu pia imetumia ubunifu kwa kiasi kikubwa. Moja ya sifa ya lugha hii ni kwamba watumizi wake ni wabunifu sana. Kwa maana kwamba kunabuniwa leksimu kila kuchao. Baadhi ya leksimu ambazo zimeingia katika lugha hii kupitia ubunifu ni pamoja na: **Mifano 17**

| **Sheng** | **Kiswahili** |
|---|---|
| *modee* | mwalimu |
| *ndula* | kiatu |
| *mbota* | Saa |
| *njeve* | baridi |
| *gondi* | mwizi |
| *rasa* | makalio |
| *zanze* | polisi |
| *mboch* | kijakazi |
| *rwabe* | shilingi mia mbili |

Kama ilivyo katika ukopaji, ubunifu wa leksimu mpya huchochewa na mabadiliko katika mazingira ya watumizi lugha kiasi cha kuingiza dhana mpya katika lugha na ikawa hakuna leksimu ya kutajia dhana hiyo. Katika hali kama hiyo watumizi lugha hubuni leksimu. Ogechi (2005:354) anasema kwamba ubunifu wa leksimu katika Sheng ni jambo lililo na mantiki ya hali ya juu. Kwa sababu hiyo kubuni leksimu katika lugha huwa ni mfanyiko ambao unaweza kufafanuliwa kiisimu. Sheng kama zilivyo lugha nyingi za ulimwengu wa tatu imejipata katika mapisi ya uvumbuzi wa kiteknolojia na hivyo kuna dhana nyingi ambazo zimeingia katika lugha hii na inawalazimu watumizi lugha hii kubuni leksimu mpya kila kunapokuwa na haja.

## 2.6 Ubadilishaji silabi

Mbinu hii japo inakosa umataifa ni njia mojawapo ambayo Sheng inatumia kujitajirisha kileksimu. Sheng hubadili silabi ambazo tayari zimo katika leksimu fulani. Ogechi (2005:340), anasema kwamba neno hukopwa kisha kurekebishwa matamshi na baadaye silabi kubadilishwa. Ngesa (2002), pia anajumlisha mbinu hii kama taratibu ya uundaji leksimu katika lugha ya Sheng; labda kutokana na uzalishaji wake. Hii ni mbinu ambayo ni aina fulani ya tabdili. Hata hivyo tabdili husababishwa mara nyingi na matamshi mabaya ilhali ubadilishaji silabi ni utaratibu wa kimaksudi ambao hutumiwa na Sheng kuunda leksimu. Sheng hubadili silabi pia kama mkakati wa kujibainisha na kuhifadhi upekee wake.

**Mfano 18**

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| card | - | kadi | - | *dika* | (kadi) |
| mother | - | madha | - | *Mudhama* | (mama) |
| story | - | stori | - | *risto* | (Hadithi) |
| bread | - | bredi | - | *dibre* | (mkate) |
| moja | - | moja | - | *jamo* | (moja) |
| nguvu | - | nguvu | - | *vungu* | (ngumu) |
| nyumba | - | nyumba | - | *mbanyu* | (nyumba) |
| mbele | - | mbele | - | *lembe* | (kufanikiwa kwa jambo) |

Kuna mfumo unaondamana na mbinu hii. Mfumo wenyewe ni kwamba kuna ukopaji wa kisemantiki katika leksimu zilizobadilishwa silabi. Japo ubia wa mbinu hii unaweza kutiliwa

shaka, ni mbinu muhimu ambayo lugha ya Sheng imedhihirisha kutumia katika kuunda leksimu zake.

## 2.7 Onomatopea

Kama wasemavyo Iribemwangi na Mukhwana (2011), onomatopea ni mbinu ya uundaji leksimu ambapo leksimu inaundwa kutokana na sifa, uamilifu, umbo, sauti au milio. Wengine husema ni uundaji leksimu kwa kuiga sauti asilia. Huu ni mchakato ambao umetumika na lugha ya Kiingereza na lugha nyinginezo za kilimwengu. Katika Kiingereza kuna leksimu kama; *buzz* (vuta kama nyuki), *hizz* (pumua kwa sauti kama ya nyoka), *bee* (nyuki) na nyingine. Vilevile Kiswahili kimepata maneno kama vile; kifagio, kifutio, patipati, pikipiki. Lugha ya Sheng pia ina mifano ambayo inaweza kuhusishwa na mbinu ya onomatopea. **Mifano 19.**

| **Leksimu** | **maana** |
|---|---|
| *bling'bling'* | vito vya chumachuma vyenye kumetameta |
| *mng'aro* | mavazi |
| *poko* | kahaba |
| *kongkodi* | utingo |
| *pang'ang'a* | kelele |
| *kacha* | pingu |

Mbinu hii haina uzalishaji mkubwa kwa lugha ya Sheng kama ilivyo kwa lugha nyingine kama Kiingereza au Kiswahili. Ni muhimu kutaja kwamba mbinu hii pia ina shida zake hasa

ikichukuliwa kwamba milio ya vitu na sifa za vitu huwa tofauti kutegemea utamaduni wa watu husika. Mathalani neno la kutajia mbwa katika Kihindi ni neno la kionomatopea tofauti na lilivyo katika tamaduni nyinginezo. Vilevile si rahisi kutoa sababu za kiisimu zinazopelekea leksimu fulani kuwa ndicho kitajwa cha kitu fulani. Kwa upande mwingine mbinu hii inaelekea kukinzana na mawazo ya Saussure (1916), kwamba hakuna uhusiano wa moja kwa moja baina ya kiashiria na kiashiriwa. Hii ni kwa sababu majina ya kionomatopea huhusishwa na dhana zinazowakilisha. Hata hivyo katika lugha nyingi ulimwenguni leksimu zinazoundwa kupitia onomatopea ni chache zikilinganishwa na leksimu nyingine kwa sababu ya unasibu wa lugha.

### 2.8. Ujenzi ghairi

Kwa mujibu wa Yule (1985), mbinu hii hutumika sana katika lugha ya Kiingereza. Ujenzi ghairi ni hali ambapo leksimu ya aina fulani (mara nyingi huwa ni nomino) inapunguzwa kimaumbo ili kuunda leksimu nyingine yenye umbo tofauti (mara nyingi leksimu undwa huwa ni kitenzi). Kupitia mbinu hii Kiingereza kimepata *televise* (tangaza kupitia runinga) kutokana na *television* (runinga), *edit* (hariri) kutokana na *editor* (mhariri) na *donate* (changa) kutokana na *donation* (mchango) miongoni mwa mengine. Mbinu hii haitumiki sana katika Kiswahili na hata katika Sheng.

Wakati mwingine ujenzi ghairi na ukatizaji hukanganya. Tofauti iliyopo ni kwamba katika ukatizaji, vipande fulani vya kifonolojia vya neno ambavyo haviwezi kufasiriwa kama neno au kiambishi hukatwa. Kwa upande mwingine katika ujenzi ghairi kipande kilichokatwa nje kinawezakutambuliwa kama neno la kujisimamia au kiambishi. Hivyo ujenzi ghairi unaweza kuwa utaratibu wa kimofolojia wa kuchanganua neno kwa misingi ya mofolojia yake ilhali

ukatizaji ni mfanyiko mahsusi wa kifonolojia unaonuiwa kufanya neno kuwa fupi kimatamshi. **Mifano 20**

| **Leksimu mpya** | **leksimu asilia** |
|---|---|
| *pang'ang'a* (kelele) | *pang'a* (kulia) |
| *wanjora* (upanga) | *wanjo* (kata) |

**2.9 Akronimu**

Katika akronimu herufi au silabi za mwanzo za neno au seti ya maneno hutumika kuundia leksimu nyingine mpya. Akronimu aghalabu huandikwa kwa herufi kubwa na hizo herufi husimamia neno fulani. Akronimu ni taratibu ya kuunda leksimu kwa kufupisha maneno yanayotumiwa pamoja kwa kuchukua herufi au silabi za mwanzo za maneno hayo, Obuchi na Mukhwana (2010:109). Sehemu za kwanza za kila neno katika kishazi huchukuliwa na kuunganishwa ili kuunda leksimu moja mpya yenye kusimamia dhana moja. Kimsingi akronimu ni mbinu ambayo imetumika sana katika Kiingereza. Mifano ya maneno yanayotokana na akronimu ni kama vile; *NATO, NASA, UNESCO, KANU* miongoni mwa mengine. Ifahamike kwamba katika akronimu baada ya kuunda leksimu, leksimu hiyo hutamkwa kama neno bali siyo kama herufi moja moja. Mbinu hii japo ni bia haitumiki katika Sheng.

**2.10. Kaleki/ tafsiri kopa**

Katika uundaji leksimu hali hutokea kwamba lugha hukopa na kutafsiri moja kwa moja au neno kwa neno. Kiingereza kimetumia mbinu hii kujipatia msamiati mwingi kutoka Kijerumani, Kifaransa na Kihispania. Kiswahili nacho kimetumia mbinu hii kupata msamiati

kama vile; mama sukari, baba sukari, Umoja wa Mataifa, ala za sauti, karamu ya mkia wa jogoo-ambayo ni tafsiri ya moja kwa moja ya; *suga mummy, sugar daddy, United Nations, speech organs, cocktail party* mtawalia. Vivyo hivyo lugha ya Sheng imejiundia leksimu *mathrii* ambayo ni tafsiri kopa kutokana na neno la Kiswahili matatu.

Mbinu hii ina matatizo yake ikiwa ni pamoja na kuleta utata wa uelewa wa maana. Ni mbinu ambayo ina utata wa kisemantiki na huenda leksimu zilizoundwa kupitia kwayo kueleweka vibaya hasa pale mzungumzaji hafahamu lugha chagizi na maana ya leksimu hizo katika lugha chagizi.

**2.11 Uhulutishaji**

Ni mchakato wa kuunganisha maneno mawili tofauti ili kuunda umbo lingine tofauti la neno. Kimsingi, mwanzo wa neno huchukuliwa na kuunganishwa na mwisho wa neno lingine ili kuunda leksimu mpya. Mathalani, neno la Kiingereza *smog* (mchanganyiko wa ukungu na moshi) linatokana na maneno *smoke* (moshi) na *fog* (ukungu), *gasohol* (mchanganyiko wa gesi na kileo) ni matokeo ya uhulutishaji wa neno *gas* (gesi) na *alcohol* (kileo) na *motel* (moteli) vilevile ni uhulutishaji wa maneno *hotel* (hoteli) na *motor* (msafara wa motokaa) kwa mujibu wa mbinu hii.

Lugha ya Kiswahili kwa upande wake pia imetumia mbinu hii kujiundia leksimu kama ifuatavyo: **Mifano 21.**

| | |
|---|---|
| chajio | chakula cha jioni |
| chamcha | chakula cha mchana |
| ukimwi | ukosefu wa kinga mwilini. |

| | |
|---|---|
| fupaja | mfupa wa paja |
| hataza | hati ya kukataza. |

## 2.12 Taratibu changamani

Hata ingawa tumezungumzia mbinu za uundaji leksimu, kila moja kwa upekee wake, ni dhahiri kwamba kuna hali ambapo mbinu zaidi ya moja inaweza kutumika ili kuunda leksimu fulani. Kwa mfano kuna hali ambapo neno linakopwa kisha linatoholewa baadaye linakatizwa na mwishoni irabu ya mwisho inaweza kubadilishwa au isibadilishwe kisha kurefushwa.

**Mifano 22.**

| **Leksimu (kopwa)** | **utohozi** | **marekebisho** |
|---|---|---|
| father | fadha | */faðɛ:/* /a/ ⟶ /ɛ/ |
| mother | madha | */maðɛ:/* /a/ ⟶ /ɛ/ |
| dirisha | dirisha | */diro:/* /a/ ⟶ /**o**/ |
| brother | bradha | */braðɛ: /* /a/ ⟶ /ɛ/ |

Japo si rahisi kubaini katika utafiti huu sababu ya kubadilisha irabu za mwisho badala ya kuwa /a/ zinakuwa /ɛ/. Katika mifano hapo juu kinachoonekana ni kwamba baada ya utohozi, neno linapomalizikia /a/ hiyo /a/ hubadilishwa na kuwa /ɛ/ ilhali baada ya ukatizaji neno linapomalizika /i/ irabu hiyo inabadilishwa na kuwa /**o**/.

## 2.13 Uambatishaji

Ni mbinu ya kuunganisha maneno mawili ambayo kwa kawaida huwa hayawi pamoja kwa mujibu wa muundo wa lugha husika ili kuunda neno jipya . Matokeo yake ni neno ambatano. Neno linalojitokeza huwa halitazamwi kama maneno mawili bali neno moja. Vilevile maana ya neno ambatano huwa siyo muungano wa maana za maneno hayo mawili yaliyotumika kuundia neno hilo. Kujua maana za maneno hayo mawili hakusaidii mtu kujua maana ya neno jipya kama wasemavyo, Fromkin na Rodman (1988:137).


Ni kutokana na mbinu hii ambapo Kiingereza kimejiundia leksimu kama *classroom* (darasa), *textbook* (kitabu cha kiada), *glassware (*vifaa vya vioo), *housegirl*(mhudumu wa nyumbani mwenye jinsia ya kike), *bedroom* (chumba cha kulala), na mengine. Kiswahili vilevile kimetumia mbinu hii na kuunda maneno kama vile *sokohuria, kionambali, changamoto, mwanamke, mwanajeshi, kitindamimba, mwanasheria* na mengine mengi. Kama asemavyo Katamba (1993:54), hii ni mbinu mojawapo ambayo ni muhimu sana katika Kiingereza na ambayo kwayo lugha hii imejitajirisha. Katika Sheng kuna leksimu kadhaa ambatano.

| **Mfano 23** | | Sheng | Maana/ Kiswahili |
|---|---|---|---|
| ambu + luma | - | *ambuluma* | - kwenda mbali |
| anda + Sika | - | *andasika* | - kutafuna miraa |
| mbara + maki | - | *mbaramaki* | - mwendawazimu (mjinga) |
| dati + gati | - | *datigati* | - ovaroli (bwelasuti) |
| buu + fee | - | *buufee* | - nauli |

## 2.14 Upolisemia / upanuzi wa kisemantiki.

Irabemwangi na Mukhwana (2011.166), wasema kwamba upolisemia ni kule kuongeza maana kwa maneno yaliyomo katika lugha. Ogechi (2005: 343), anasema kuwa nomino kopwa katika Sheng hupata upanuzi wa kisemantiki. Ogechi, huku akitoa mfano wa leksimu kama vile *chuo* anasema kwamba neno *chuo* limekopwa kutoka Kiswahili. Katika Kiswahili *chuo* lina maana ya *college* kama linavyoeleweka katika Kiingereza lakini katika Sheng *chuo* lina maana ya shule ya msingi, shule ya upili, chuo cha anuai na chuo kikuu. Hivyo kimsingi neno *chuo* limepata upanuzi wa kisemantiki. Leksimu nyinginezo ambazo zimepata sifa ya upolisemia ni pamoja na; *mzee, teke, keja.* Kinachojitokeza katika Sheng ni kwamba ukopaji leksimu huandama na ukopaji wa kisemantiki. Pia kutokana na ukopaji wa kisemantiki ndipo kunakuwa wazi kwamba kumetokea upanuzi wa kisemantiki.

Pamoja na kwamba mchakato huu umechukuliwa kama mbinu ya uundaji leksimu vile vile ni mchakato wa pragmatiki leksika. Upanuzi kama huo wa leksimu *chuo* unaweza kuwasilishwa kama upanuzi chini ya pragmatiki leksika kama ifuatayo:




**Kielelezo cha 5: Upanuzi wa kisemantiki**

## 2.15 Unyumbuzi kapa

Katika mchakato huu, leksimu hubadilisha kategoria bila kuambishwa wala kufanyiwa chochote cha kubadili umbo la leksimu hiyo. Hivyo leksimu ambayo ni nomino linaweza kutumika kama kitenzi. Mbinu hii pia huitwa ubadilishaji amilifu. Katamba (1993:54), anasema kwamba leksimu mpya inaweza kuundwa bila kubadili umbo la leksimu asilia. Kwa kiwango fulani muundo wa kimofolojia wa neno na nafasi iliyochukuliwa na neno hilo katika tungo husaidia kujua kama neno hilo ni nomino au kitenzi. Unyumbuzi kapa huchukuliwa kama aina fulani ya uambishaji, japo ni uambishaji usiodhihirika kimofolojia. Hivyo hata ingawa leksimu haiwi na viambishi kiothografia, huwa inachukuliwa kwamba viambishi hivyo ni kapa, Adams (1973).

Unyumbuzi kapa au ubadilishaji amilifu ni mbinu ambayo lugha ya Kiingereza hutumia mara kwa mara hasa katika utungo. Kwa mfano katika mifano ifuatayo neno *chair* ni nomino na *kitenzi* mtawalia.

i. *The chair of the meeting* (mwenyekiti wa mkutano).
ii. *John will chair the meeting.* (John ataongoza mkutano).

Lugha za kibantu ni lugha ambishi bainishi, na hivyo ili kategoria ya neno ibadilike huwa kunaongezwa viambishi nyumbuzi kama vile vinominishi. Labda kutokana na sababu hiyo mbinu hii inaonekana kutopendelewa na Kiswahili na hata Sheng.

## 2.16 ubadilishaji rajamu kuwa maneno kamili.

Majina ya bidhaa hutumika na kuzoeleka hivi kwamba watumizi lugha huchukua majina hayo na kuyafanya kuwa majina kamili. Hii ni mbinu ambayo hutumika sana katika lugha ya mazungumzo ambapo rajamu fulani fulani (majina ya bidhaa), yanaaza kupokezwa sifa za nomino au vitenzi kamili. Kwa mfano rajamu kuanza kuambishwa viambishi vya njeo, hali, nafsi na vitambulishi vya wingi. Kuna jina la huduma ya utumaji ujumbe kutumia rununu ambalo limekuja kubadilishwa na kutumika kama neno kamili. *SMS* ni akronimu ya *short message service* (ujumbe mfupi). Akronimu hiyo imepata sifa ya neno kamili.

Katika mazungumzo mara nyingi watu hutumia neno *sms* kama kitenzi ambacho kinaweza kuambishwa kwa namna mbalimbali. Hivyo kuna maneno kama; *sms-ing, sms-ed, sms-es.* Mbinu hii japo si maarufu sana inatumika katika miktadha mbalimbali ya matumizi lugha. Hakuna mifano katika data tuliyokusanya inayoweza kuashiria kutumika kwa mbinu hii katika Sheng.

## 2.17 Hitimisho

Uundaji leksimu katika lugha huchangiwa na sababu nyingi. Kuna sababu za kiisimu na zisizo za kiisimu. Sababu mojawapo ya kiisimu ni mahitaji ya kileksimu- ambapo kuna dhana mpya ambayo imeingia katika lugha na ikawa hakuna leksimu ya kutajia dhana hiyo. Sababu nyinginezo ni mabadiliko ya kiteknolojia, utangamano na tamaduni geni, dhana mpya za kidini na urejelezi kwa mambo mapya ya kutajia mimea na wanyama. Hivyo katika kila lugha hali hutokea ambapo kuna hitaji la kuunda leksimu mpya.

Lugha nyingi ulimwenguni hutumia mikakati mbalimbali kuunda leksimu hitajika. Kila lugha huweza kutumia baadhi ya mbinu tulizojadili hapo juu. Ifahamike kwamba hali hutokea kwamba lugha inapendelea mbinu fulani fulani. Mathalani Kiingereza kimejitokeza tangu zamani kupendelea ukopaji, uambishaji, uambatishaji na akronimu kuliko mbinu nyinginezo. Hata hivyo hiyo siyo kusema kwamba mbinu nyinginezo hazitumiki katika Kiingeraza, bali mbinu hizo zina uzalishaji wa hali ya juu kuliko mbinu nyinginezo kama asemavvyo, Katamba (1993).

Katika Kiingereza misamiati mingi kutoka Kigiriki, Kilatini, Kijerumani, na kutoka lugha nyingine za Kirumi imekopwa kupitia Kifaransa, Hock & Joseph (1996). Vivyo hivyo Sheng imekopa kutoka lugha nyingi lakini kupitia Kiswahili. Leksimu kutoka lugha chagizi inaingizwa katika Kiswahili, kuhawilishwa na kisha kuchukuliwa na Sheng.

Kama ambavyo imejitokeza katika sehemu iliyopita, kifupi tunaweza kusema yafuatayo:

1. Sheng huunda leksimu zake kama zilivyo lugha nyingine za kilimwengu. Michakato ambayo inapendelewa na lugha hii ni pamoja na; ukopaji, ubunifu, ukatizaji, uambishaji, upolisemia (upanuzi wa kisemantiki), ubadilishaji silabi, uambatishaji na onomatopea.

2. Leksimu za Sheng hupitia michakato zaidi ya moja hadi kufikia hali yao katika Sheng. Huu ni mfanyiko ambao katika sehemu iliyopita inaitwa mbinu changamano.

3. Pale ambapo kuna ukopaji wa leksimu kutoka lugha chagizi, ukopaji huo huandamana na ukopaji wa kisemantiki. Hata hivyo katika baadhi ya leksimu kopwa kuna upanuzi wa kisemantiki ulio dhahiri.

4. Japo Sheng bado inatiliwa shaka hasa uasilia wake, jambo ambalo ni wazi kupitia mbinu za uundaji leksimu ni kwamba inazidi kukua kileksimu na hivyo pia kisemantiki.

5. Sifa mojawapo ya lugha ya binadamu ni ubunifu. Maneno mageni huzidi kuongezeka katika kamusi ya kiakili za watumizi lugha. Kunapokosekana leksimu watumizi lugha hutia juhudi kupitia mbinu mbalimbali kuunda leksimu hiyo. Sheng haijawachwa nyuma kwa mfanyiko huo muhimu wa kiisimu kama ilivyojitokeza.

Baada ya leksimu kuundwa katika lugha, leksimu hizo huwa si tuli kisemantiki bali hupitikiwa na mabadiliko ya kisemantiki. Katika sura ifuatayo tunashughulikia maendeleo ya kisemantiki kwa ujumla. Kama kigezo kikuu cha maendeleo hayo tunazungumzia mabadiliko ya kisemantiki, aina, sababu na mchango wa muktadha katika mifanyiko hiyo.

## SURA YA TATU

## 3.0 MAENDELEO YA KISEMANTIKI NA UFASIRI WA NADHARIA YA PRAGMATIKI LEKSIKA.

### 3.1 Utangulizi

Katika sura hii tumezungumzia mabadiliko ya kisemantiki kama njia mojawapo ya maendeleo ya kisemantiki. Aidha tumetumia nadharia ya pragmatiki leksika inapotosheleza kwa ufafanuzi. Tumefanya hivyo kwa kutambua kwamba njia mojawapo ya ukuaji wa lugha ni kubadilika kwake. Kama anavyosema Singleton (2000:143), mabadiliko ya kisemantiki yanayokumba leksimu mahsusi hayawi ya kinasibu kwa ujumla, bali kuna hali fulani ambazo huchochea mabadiliko hayo ya kuhamisha maana za leksimu. Singletone anazidi kusema kwamba kuna michakato mahsusi ambayo husababisha maendeleo ya kisemantiki ya lugha. Katika utafiti huu maendeleo ya kisemantiki ni dhana ambayo inatumika kumaanisha hatua fulani ambayo lugha hupiga katika kujiimarisha kimaana ili kufaulisha mawasiliano. Hivyo leksimu hubeba maana na itokeavyo kwamba kuna mabadiliko ya kimaana yanayokumba leksimu hiyo, mabadiliko hayo yawe ni katika upanuzi wa kimaana au ubanifu, huchukuliwa kama maendeleo ya aina fulani ya kisemantiki.

Lugha inapojiimarisha kimaana, inaweza kubuni leksimu mpya zenye kubeba dhana mpya au leksimu zilizoko kupata fahiwa nyongeza au kupunguza sehemu za maana. Mifanyiko kama hiyo huweza kuashiria maendeleo ya kisemantiki ya lugha hiyo. Ni hali kama hiyo inayopitikia lugha ya Sheng. Data tunayotumia hapa imejumlisha ile tuliyokusanya kutumia hojaji na zaidi ni ya mahojiano. Wahojiwa wengi walikiri kwamba Sheng ni lugha inayokua sana kisemantiki na jambo hilo ni wazi kutokana na jinsi Sheng inavyojibunia leksimu kila

kuchao. Kwa kuchanganua data kwa makini leksimu za Sheng zinadhihirisha mabadiliko mengi ya kisemantiki ambayo nadharia ya pragmatiki leksika inaweza kufafanua vyema. Vilevile wahojiwa walitoa mifano mingi ya leksimu za Sheng ambazo kwa sasa zinatumika kwa maana zilizo tofauti na maana zao za awali.

Lugha ya Sheng inazidi kuendelea kileksimu, Shitemi (2002), na hivyo kisemantiki pia. Katika utafiti huu tulinuia kubaini kama kuna maendeleo ya kisemantiki kupitia ubunifu wa kileksimu katika Sheng. Aidha tulitaka kubainisha kama kuna mchango wowote wa kimuktadha katika ubunifu wa kileksimu na kubaini mfumo wowote wa kisemantiki unaodhihirika. Mabadiliko ya kisemantiki ni kigezo kikuu katika maendeleo ya kisemantiki na hivyo katika sehemu ifuatayo tunashughulikia mabadiliko ya kisemantiki kwa kutoa mifano ya lugha ya Sheng. Kama ambavyo ni wazi kufikia hapa, Kiswahili kimetumika kama lugha kienzo katika kazi hii, na ikitokea kwamba mifano ya Kiswahili imetolewa tumefanya hivyo ili kufafanua zaidi hoja fulani. Pamoja na kwamba mabadiliko ya kisemantiki yanadhihirisha maendeleo ya kisemantiki pia mabadiliko hayo huchangia ubunifu wa kileksimu.

### 3.2 Mabadiliko ya kisemantiki.

Mabadiliko ya kisemantiki, kama yale ya kileksimu hutokea kwa sababu ya ubunifu wa kileksimu katika lugha, kuwepo kwa mabadiliko ya kimaana ya leksimu na hata wakati mwingine kupotea kwa leksimu fulani na leksimu nyingine kubuniwa. Aidha leksimu za zamani kupata uhuisho kwa maana mpya na leksimu nyingine kupata vivuli vingine vya fahiwa, Ullmann (1962:195) .

Kama yalivyo mabadiliko ya kifonolojia, muktadha huchangia mabadiliko hayo ya kisemantiki. Mabadiliko ya kisemantiki hutanguliwa na uhamishaji au ugeukaji wa kisemantiki. Wakati wa kuhamisha maana ya leksimu kutoka maana A hadi maana B, maana zote mbili hutumika kwa wakati mmoja katika lugha husika aghalabu kwa muda fulani. Mfano mzuri ni ule wa leksimu 'shoga' katika Kiswahili. Maana bora ya leksimu hii ni rafiki wa kike wa mwanamke. Maana nyingine ya leksimu hii ni 'msenge'. Maana hizi zote zinatumika kwa wakati mmoja lakini ile maana yenye hisia mbaya ya msenge inashika zaidi na hivyo baada ya muda watumizi lugha wataishia kujitenga na kutumia leksimu 'shoga' kwa maana ya rakifi wa kike. Mabadiliko ya kisemantiki ni mifanyiko ambayo hukumba lugha yoyote ya binadamu kama mfano wa leksimu 'shoga' unavyodhihirisha. Kwa sababu hiyo, siyo mifanyiko ya kipekee kwa lugha ya Sheng bali hukumba lugha zote.

Kwa kifupi, kama Fromkin na Rodman (1988), Arlotto (1972) na Ullmann (1957) wana maoni yenye kukaribiana, kwamba leksimu hubadili maana zao mara kwa mara kupitia mapisi ya wakati wa matumizi. Trask (1994: 41), anasema kwamba kama ilivyo katika vipengele vingine vya lugha, maana za leksimu hubadilika baada ya muda fulani. Kazi ya awali kabisa ambayo iliwahi kudokeza mabadiliko ya kisemantiki ni ya Trier (1934) kama anavyonukuliwa katika Palmer (1981). Mtazamo wa Trier ulionyesha jinsi mfumo wa kisemantiki wa vikoa vya maana unavyoweza kubadilika baada ya muda. Leksimu huweza kujitofautisha kimaana na kuondoka katika kikoa fulani cha maana hadi kingine. Wataalamu wengi huainisha aina mbalimbali za mabadiliko ya kisemantiki. Hata hivyo, kama anavyosema Arlotto (1972:176), kuna aina nyingi sana za mabadiliko ya kisemantiki. Kuna aina zenye kukita katika isimu na zile zilizo nje ya mawanda ya isimu. Sehemu ifuatayo inashughulikia aina zilizokita katika mawanda ya isimu, kwa maana kwamba zinaweza kufafanuliwa kwa misingi ya kiisimu.

Akmajian et al (2001), Trask (1994), kama alivyo Arlotto (1972), wanaainisha aina za mabadiliko ambayo tumeshughulikia katika sehemu ifuatayo.

### 3.2.1 Upanuzi

Trask (1994), anasema kwamba katika matumizi lugha hali hutokea kwamba leksimu inatumika kwa maana ya kijumla zaidi. Arlotto (1972:177), naye anasema kwamba upanuzi hutokea pale ambapo vitu vinavyomaanishwa na leksimu fulani vimeongezeka. Anachosema Arlotto ni kwamba leksimu inapopata nyongeza za fahiwa, leksimu hiyo hukumbwa na upanuzi wa kimaana hivyo leksimu hiyo huweza kutumika kumaanisha vitu vingi. Upanuzi huwezesha matumizi mapana ya leksimu katika lugha. Leksimu nyingi katika Sheng zina matumizi mapana kifahiwa. Kunapokuwa hakuna leksimu ya kutajia kitu fulani na mradi kuna leksimu ya fahiwa iliyo karibu na leksimu hiyo, upanuzi wa aina fulani hutokea. Kwa upande moja upanuzi kama huo unaweza kuchukuliwa kama njia ya uzibaji mwanya wa kileksika.

Aitchison (2002:151), huku akilinganisha leksimu na nambari anasema kwamba, leksimu tofauti na nambari, haziwi na maana moja tu mahsusi isiyobadilika. Leksimu katika lugha hupata upanuzi wa kisemantiki. Fromkin na Rodman (1988), nao wanasema kuwa upanuzi wa kisemantiki hutokea pale ambapo leksimu inachukua maana ya kijumla zaidi kuliko ilivyokuwa ikimaanisha hapo awali. Watumizi lugha hujua maana za kiensaiklopidia za leksimu fulani lakini katika matumizi leksimu hupatiwa maana za kijumla na mara nyingi maana hizo huwa zimekiuka maana za kiensaiklopidia. Jambo hili huchochewa na muktadha kama tutakavyoona baadaye.

**Mfano 24a** : *Chali wa ocha ameishia.*

Mwanaume wa mashambani ameondoka (tafsiri).


**24b**: *Modee ameishia chuo.*

Mwalimu ameenda shuleni (tafisri).

**24c**: *Magava wamesleki baro.*


Polisi wamezubaa barabarani (tafsiri).

Habari hii inaweza kuwasilishwa kwa kielelezo cha upanuzi kama hiki kifuatatao:




**Kielelezo 6: Upanuzi wa kimaana: Kutoka [PLIN 3001] 2006-07**

Kama wasemavyo Fromkin na Rodman (1988:315), kwamba leksimu inapopanuka kisemantiki, leksimu hiyo humaanisha vitu vyote ilivyokuwa inamaanisha awali kisha kupata nyongeza za maana, leksimu *chali* (24a) imepanuliwa zaidi kimaana. *Chali* katika Sheng humaanisha mpenzi wa kiume. Lakini matumizi ya hapo juu yamepanuliwa na kupata maana ya kijumla zaidi na hivyo inamaanisha 'mwanaume' kwa ujumla. Katika hali hiyo leksimu hiyo imepanuka kimaana hivi kwamba ile dhana ya 'uanaume' bado ipo na kisha kuna fahiwa zaidi. Mifano 24b, inadhihirisha upanuzi wa kisemantiki kwa sababu leksimu *chuo*, ilivyotumika inajumlisha aina zote za shule. Hali kadhalika 24c leksimu *gava* imetumika kwa fahiwa ya kijumla, kwamba inamaanisha polisi bila kubainisha kama ni kitengo kipi cha polisi. Vilevile *gava* bado ina fahiwa ya utawala. Kielelezo kifuatacho ni cha upanuzi wa nyongeza ya fahiwa.




**Kielelezo cha 7: Nyongeza za kifahiwa**

### 3.2.2 Kubanika kisemantiki.

Kama tulivyokwisha arifu msisitizo wetu uko kwenye upanuzi wa kileksika, hata hivyo hapa tumezungumzia ubanifu wa kisemantiki kwa sababu leksimu inapobanwa kisemantiki matokeo ni ubunifu wa kileksimu. Kama asemavyo Arlotto (1972:170), leksimu hubanwa kisemantiki pale ambapo leksimu hiyo inapunguza baadhi ya maana zake na kuishia kuwa na maana mahsusi. Mfano mzuri wa leksimu ya Sheng ni *ngoma*; leksimu hii awali ilitumika kumaanisha muziki kwa ujumla. Lakini baada ya kanda zenye kurekodiwa kuwa maarufu sana, leksimu *ngoma* ikaanza kutumika kumaanisha muziki unaochezwa katika ukumbi ulio wazi ilhali muziki uliorekodiwa studioni huitwa *mahewa*. Kubanika kwa maana ya leksimu *ngoma* kwa kiasi fulani kumechangia ubunifu wa kileksimu ambao matokeo yake ni leksimu *mahewa.* **Mfano 25.**

*a) Tuliishia ngoma Kanii.*

Tulienda kucheza muziki *Carnivore* (tafsiri).

*b) Mazee kuna mahewa kwa mbanyu.*

Jamaa, kuna muziki kwa nyumba (tafsiri).

*c) Masa ameniwahi ganji.*

Mama amenipa pesa (tafsiri).

Mfano 25a, unafasiriwa kumaanisha muziki unaochezwa na waimbaji wanatazamwa waziwazi kwenye ukumbi ilhali 25b unamaanisha muziki unaosikika ukichezwa kwenye redio au kaseti kutoka kwenye kanda fulani iliyorekodiwa. Hata hivyo maana ya awali ya leksimu *ngoma* bado haijapotea kabisa na baadhi ya watumizi Sheng huitumia japo fahiwa hiyo imepunguka. Kulingana na utafiti wa nyanjani, leksimu *-wahi* katika 25c humaanisha; kupatia mtu kitu, kupiga mtu, kushinda mtu katika masomo au utekelezaji wa kitu. Hata hivyo kulingana na matumizi ya 25c leksimu *–wahi* imebanwa kumaanisha 'kupatia mtu kitu'. Muktadha umeruhusu ufasiri mmoja tu.

### 3.2.3 Matumizi ya kitamathali

Hii ni aina nyingine ya mabadiliko ya kisemantiki. Mara nyingi leksimu hupata maana nyongeza kupitia matumizi ya kitamathali. Akmajian et al (2001), wanasema kwamba leksimu hupata maana zaidi kupitia matumizi ya kitamathali ya leksimu hiyo. Tunakumbusha kwamba katika nadharia ya pragmatiki leksika matumizi ya kitamathali ni mojawapo ya mchakato wa upanuzi wa kileksika. Ni muhimu kukumbuka kwamba mabadiliko ya kisemantiki ya leksimu hutokana pia na matumizi ya kitamathali ya leksimu. Leksimu inapotumika kitamathali, baada ya muda fulani maana hiyo huzoeleka na mwishowe kuchukuliwa kama maana ya kawaida ya leksimu hiyo. Arlotto (1972), kama Lyons (1977), na Akmajian (2001), anachukulia matumizi ya kitamathali kama aina ya mabadiliko ya kisemantiki yanayokumba leksimu katika lugha. Aidha Singleton (2000:145) anasema kuwa matumizi ya kitamathali ni suala kuu la kusababisha mabadiliko ya kisemantiki.

**Mfano 26.**

a) *Machali humanga mamanzi.*

Wanaume hujamiiana na wasichana (tafsiri).

*b) Mafala wamelipua noma.*

Wajinga wamesababisha machafuko (tafsiri).

*c) Mshii amedandia mathrii.*

Msichana amepanda matatu (tafsiri).

Katika Sheng leksimu *manga* huwa na maana ya kula chakula. Lakini katika mfano 26 hapo juu leksimu hiyo imetumika kitamathali na kwa hivyo inamaana ya kufanya mapenzi au kujamiiana. *Lipua* kwa upande wake humaanisha kufanya jambo nje ya majukumu au kupita kiasi. Katika matumizi ya 26b maana iliyosimbwa ni ya kitamathali na hivyo maana ya 26b ni 'kusababisha kitu kutendeka.' *Dandia* kikawaida humaanisha kushikilia kitu kwa mikono, lakini matumizi ya *dandia* katika 26c ni ya kitamathali. Kwa sababu hiyo maana ya *dandia* 26c ni 'kupanda'.

### 3.2.4 Uhamishaji wa maana

Kuna wataalamu ambao pia wanajumlisha uhamishaji maana kama aina ya mabadiliko ya kisemantiki. Radford et al (1999), wanasema kwamba maana ya leksimu katika lugha huweza kuhamishwa. Leksimu huweza kupoteza maana yake ya asili na kupatiwa maana nyingine mpya lakini ambayo ina ukaribu na ile maana ya awali. Jambo hili huweza kutokea kwa ajili ya umbuji wa dhana za kidharura katika akili ya mtumizi lugha fulani. Katika pragmatiki leksika umbuji wa dhana za kidharura husaidia kujenga chukulio ambazo husaidia ufasiri wa maana katika muktadha kama wasemavyo Sperber na Wilson (2002). Uhamishaji maana kama ulivyotumika hapa una maana kuwa leksimu inapatiwa maana nyingine ambayo siyo maana yake kikawaida. Katika lugha ya Sheng kuna leksimu ambazo zimekopwa kutoka

lugha nyingine na kisha maana zao kuhamishwa kabisa. Kwamba badala ya leksimu kuhifadhi maana yake iliyokuwa nayo katika lugha chagizi maana hiyo huhamishwa na leksimu hiyo kupata maana nyingine tofauti. **Mfano 27.**

*a) Masa amedunga mngaro poa.*

Mama amevalia nguo nzuri (tafsiri).

*b) Buda amechizi noma .*

Baba amechanganyikiwa (tafsiri).

c) *Sikunyita gidhafu poa.*

Sikuelewa hesabu vizuri (tafsiri).

Leksimu ya Sheng *dunga* ni leksimu mkopo ambayo humaanisha kuchoma kwa kutumia kifaa chenye ncha pia humaanisha kutoboa. Lakini katika mfano 27a maana yake imehamishwa na kupatiwa maana nyingine ambayo ni kuvaa. Ikumbukwe kwamba kuna uhusiano wa kidhana baina ya kudunga na kuvaa na uhusiano huo ndio umetumika katika uhamishaji maana. Maana ya leksimu *–chizi* imehamishwa kama katika 27b na hii leo leksimu hiyo badala ya kumaanisha mwendawazimu, inamaanisha mtu aliyechanganyikiwa au mtu asiye na mpangilio katika kutenda mambo yake. Ili kuwa na ubainishi, leksimu *mwenda* ndiyo sasa inatumika kwa maana ya mtu mwenye akili punguani. Hali ya uhamishaji maana pia inaweza kusemwa kwa leksimu *–nyita.* Leksimu hii ilikopwa kutoka Kikikuyu kwa maana ya kushika kitu kutumia mikono. Katika muktadha wa matumizi ya 27c maana yake imehamishwa kabisa na ufasiri wake ni 'kuelewa.'

### 3.3 Mabadiliko ya kisemantiki kama michakato ya pragmatiki leksika.

Mabadiliko ya kisemantiki yanaweza kufafanuliwa zaidi kama michakato ya kipragmatiki leksika. Hii inatokana na ukweli kwamba mabadiliko hayo hupata motisha kutokana na muktadha- uwe wa kiisimu au wa hali halisi katika ulimwengu wa watumizi.

Katika historia ya mabadiliko ya kisemantiki, kama pangehitajika muhtasari wa michakato hiyo yote, labda ufinyu wa kisemantiki ungesheheni muhtasari huo kuliko michakato yoyote ile. Lakini kama ambavyo tutaona katika sehemu zifuatazo mchakato wa upanuzi wa kisemantiki unajumlisha michakato mingineyo ambayo ni muhimu sana katika kazi hii. Mabadiliko ya kisemantiki yamekuwepo toka jadi, (Hock na Joseph 1996) hata kifungu hiki katika bibilia kinaweza kudokeza mabadiliko hayo.

> *Hapo mwanzo kulikuwa na neno, na neno lilikuwa na Mungu na neno lilikuwa Mungu.*

Kutokana na nukuu hiyo ambayo ni kifungu cha kibiblia kulingana na Yohana mtakatifu sura ya kwanza mstari wa kwanza, kunaweza kuchukuliwa kuwa mwanzoni kulikuwa na neno moja tu na ambalo kwalo maneno yote yametokana nalo. Japo hakuna haja hapa ya kurejelea asili ya lugha ambayo ina maelezo mengi ya kukinzana kinadharia, huenda lugha ya kwanza kuwahi kutumika na binadamu ilikuwa na leksimu chache tu za haja ambazo zilitumika kutajia vitu vilivyokuwemo katika ulimwengu wakati huo. Kutokana na nukuu hapo juu huenda leksimu moja ilikuwa na fahiwa pana sana kimaana. Upana huo wa kimaana huweza kufafanuliwa vyema kama mchakato wa kipragmatiki leksika (tazama 3.2.1). Vivyo hivyo, huweza kusemwa kuhusu Sheng, kwamba huenda leksimu za Sheng zilikuwa chache lakini baadaye zikazidi kukua na mwishowe kuimarisha semantiki ya lugha hii.

### 3.3.1 Upanuzi wa Kileksika kama mchakato wa pragmatiki leksika

Kama tulivyokwisha arifu awali, katika utafiti huu tumekita zaidi katika upanuzi wa kileksika ambao ni mchakato mojawapo wa nadharia ya pragmatiki leksika. Aidha katika mchakato huu kuna michakato mingineyo tunayozungumzia lakini msisitizo ukiwa kwenye ubunifu wa kileksimu. Ubanifu wa kileksika kwa upande wake ni pale ambapo leksimu inatumika kwa maana iliyo finyu zaidi kuliko maana iliyosimbwa katika sarufi. Upanuzi wa kileksika ambao ndio mahusiko ya sehemu hii ni matumizi ya leksimu katika upana wake kimaana. Ifahamike pia kwamba kiwango cha ubanifu wa kileksika kinategemea sana utafutaji wa uhusiano. Hivyo maana iliyosimbwa ikiwa jumla sana kuzidi matarajio ya msikilizaji hasa katika tukio la usemi, msikilizaji hulazimika kufanya ubanifu zaidi. Msikilizaji hufanya hivyo hadi afikie maana iliyowasilishwa au hadi pale tamko linapofikia uhusiano ufaao.

Ufasiri wa maana katika hali kama hiyo utahusisha umbuji wa dhana za kidharura katika akili-jambo ambalo hutegemea muktadha zaidi. Katika upanuzi wa kileksika, leksimu hutumika kuwasilisha vitu na matukio ambayo kimsingi hukiuka maana zilizosimbwa kiisimu za leksimu hiyo. Upanuzi wa kileksika kama ilivyo ubanifu wa kileksika huchochewa na utafutaji wa uhusiano na vilevile huhusu umbuji wa dhana za kidharura, umbuji huo hata hivyo unakita katika habari zilizomo kwenye ensaiklopidia ambazo ni maana simbwa za dhana hiyo. Kimsingi katika mchakato wa upanuzi, habari zilizo kwenye ensaiklopidia ni muhimu maanake ndizo hutumiwa kama kianzilio cha upanuzi na kisha habari za kimuktadha husaidia kujaliza na kufanikisha upanuzi huo, Blutner (2000), Carston ( 2002), Wilson na Sperber (2002). Hivyo maana ya leksimu siyo tu orodha ya fasili na ufafanuzi wa kikamusi kama inavyochukuliwa na wanasemantiki leksika bali orodha hiyo ni muhimu na vilevile muktadha ni muhimu katika kufasiri maana za leksimu. Kama wanavyodai Sperber na Wilson

(1995:86), maana ya leksimu ni dhana na dhana huwa na sifa za kimantiki, (mantiki hapa ina maana ya seti ya kanuni za virejelewa vinavyohusu uhusiano wa dhana na dhana nyingine). Kwa sababu hiyo kuna urejelezi kwenye akili ambao hufanywa na mtumizi lugha ili kufasiri maana. Dhana, kama wasemavyo Sperber na Wilson (1995), ni kifaa cha kisaikolojia kilicho na uwezo wa kufikia habari zilizohifadhiwa akilini. Habari hizo huhifadhiwa kama fremu, skimu, miswada na mipangilio fulani katika akili za watu. Kwa sababu hiyo tofauti kati ya habari za kimantiki na zilizo kwenye orodha ya ensaiklopidia ni muhimu katika kufanya upanuzi ufaao katika muktadha ufaao.

Kuna aina mbalimbali za upanuzi wa kileksika ambazo ndizo tunazungumzia katika sehemu ifuatayo.

#### 3.3.1.1 Ukisivu wa Kimaana

Hii ni aina ya upanuzi wa kileksika kwa mujibu wa Lasersohn (1999). Lasersohn anasema kwamba, ukisivu wa kimaana hutokea pale ambapo leksimu hutumika kutajia vitu vingi ambavyo kimsingi viko nje ya maana zilizosimbwa kiisimu.

**Mfano 28.**

a) *Kuishia Nyeri kwa buu ni rwabe.*


Kwenda Nyeri kwa gari ni shilingi mia mbili (tafsiri).

b) *Magava hutuna baro.*

Polisi hulala barabarani (tafsiri).

Katika mfano 28, leksimu *buu* na *rwabe* zimetumika kwa ukisivu tu. Maana ya *buu* inaweza kupanuliwa na hivyo kukisiwa kumaanisha aina yoyote ya gari mradi gari hilo linasafirisha

abiria hadi Nyeri. Vilevile leksimu *rwabe* humaanisha shilingi mia mbili pesa za Kenya. Nauli huweza kubadilikabadilika kutegemea hali ya anga na saa za usafiri na hivyo leksimu *rwabe* hapo juu inaweza kufasiriwa kwa ukisivu wake. Upanuzi kama ulivyo ubanifu hutegemea muktadha. Kwa sababu hiyo leksimu moja inaweza kupanuliwa au kubanwa kwa viwango mbalimbali kutegemea muktadha wa matumizi kama anavyosema Lewis (1979). Leksimu nyingine ambayo imetumika kwa ukisivu ni *tuna* katika 28b. leksimu *tuna* humaanisha 'kulala' lakini katika 28b maana yake inaweza kukisiwa kumaanisha 'kuzubaa'. Ukisivu unaweza kuwasilishwa kwa kielelezo kifuatacho.





**Kielelezo cha 8: Ukisivu: Kutoka [PLIN 3001] 2006-07**

### 3.3.1.2 Tamathali kama upanuzi wa kileksika.

Grice (1989), anachukulia tamathali kama ukiukaji mkubwa wa kanuni ya ukweli na kwamba ukiukaji huo ndio husababisha umaanisho. Hivyo kulingana na nadhana ya Grice, ambaye anachukuliwa kama mwanzilishi wa pragmatiki mamboleo, matumizi ya tamathali katika usemi hukusudiwa kuzua umaanisho. Msikilizaji anafaa kuchukulia kwamba mzungumzaji anayekiuka kanuni ya ukweli au kanuni yoyote ile katika orodha ya kanuni alizotoa Grice, hunuia kuzua umaanisho ambao unahusishwa na propozisheni za kweli. Katika pragmatiki leksika tamathali huchukuliwa kama aina ya upanuzi wa kileksika kwa sababu inamlazimu msikilizaji kufanya upanuzi fulani wa leksimu ili afasiri maana vyema. Katika mchakato huu leksimu hutumika kwa hali ambapo maana inayowasilishwa huonekana kuondoka nje kabisa ya ile maana iliyosimbwa. Kwingineko katika semantiki leksika tamathali ni ukiushi mkubwa

wa kanuni za kisemantiki. Kielelezo kifuatacho kinafafanua michakato ya upanuzi wa kitamathali.

**Mfano 28:** *Kumanga manzi si poa.*




**Kielelezo cha 9: Tamathali kama upanuzi:** [PLIN 3001] 2006-07

*Kumanga manzi si poa.*

Maana:

i) Kula msichana si kuzuri.

ii) Kujamiiana na msichana si kuzuri.

iii) Kufanya mapenzi na msichana si kuzuri.

Maana ya tatu ambayo ni; kufanya mapenzi, inaafiki zaidi matumizi ya kitamathali ya leksimu *manga.* Kikawaida leksimu hiyo humaanisha; kula chakula kama vile; *kumanga dishi.* Katika mfano wetu hapo juu, leksimu *manga* imetumika kitamathali na inambidi mtu kufanya upanuzi wa kiasi fulani ili kujitokeza na ufasiri ufaao. Maana i, ii, iii, zinaweza kuchukuliwa kama ndizo alizo nazo mtumizi lugha ya Sheng na ndizo anaweza kuzifikia kila anaposikia neno *manga.* Maana leksika inahusisha leksimu *manga* na dhana *MANGA*, kisha uhusiano huo ndio unaofikia habari za kimantiki na za kiensaiklopidia. Mwisho ufasiri unaofikiwa ni ule wa (iii) kufanya mapenzi katika muktadha huo. Jambo hilo huwezeshwa na upanuzi anaofanya msikilizaji.

### 3.3.2 Muktadha kama kipengele cha pragmatiki leksika.

Imejitokeza katika utafiti huu kwamba muktadha huchangia pakubwa ubunifu wa kileksimu. Aidha upanuzi wa kileksika ni mchakato uliokita kwenya muktadha, hivyo imekuwa bora kuzungumzia dhana ya muktadha. Muktadha ni muhimu hivi kwamba pragmatiki huweza kufafanuliwa kama uchunguzi wa maana ya neno kwa mujibu wa muktadha. Kwa sababu hiyo wataalamu wengi wa isimu hukubaliana kuwa pragmatiki ni uchunguzi wa maana kwa mujibu wa muktadha wa matumizi neno. Blutner (2000), anasema kwamba ufasiri wa maana ya leksimu au tamko lolote hutegemea muktadha, elimu na maarifa aliyo nayo msikilizaji au msemaji kuhusu mazingira yake. Hata hivyo muktadha ni dhana pana na hurejelea mambo na vitu vingi.

Katika matini, muktadha huchukuliwa kama sentensi zinazotangulia leksimu fulani na zile zinazoifuata. Hivyo katika mtazamo huo, maana ya leksimu fulani ni jumla ya mambo yanayozingira leksimu hiyo katika matini, Beaugrande na Dressler (1981). Kwa upande mwingine muktadha hujumlisha mambo ya kihalisia katika ulimwengu wa watumizi lugha. Kifupi kuna muktadha wa kiisimu na muktadha ulio nje ya mawanda ya isimu (muktadha halisi kv; watu, majengo, wakati, kumbukizi, utamaduni nk.)

Muktadha vilevile unaweza ukaainishwa kama muktadha wa kisaikolojia. Muktadha unapotazamwa kama dhana katika akili huwa kinachorejelewa ni habari za kiensaiklopidia zilizohifadhiwa kwenye akili, Sperber na Wilson (1995). Kutokana na habari zilizohifadhiwa kimantiki katika akili za watumizi, mtumizi lugha huwa na uwezo wa kujitokeza na chukulizi za kijumla kuhusu muktadha wa usemi. Hivyo katika tukio la usemi chukulizi za kijumla huweza kubanwa ili kupata muktadha ufaao wa kufasiri maana ya leksimu fulani kama ilivyotumika. Ili kubana maana ya leksimu fulani, kupanua maana ya leksimu, kukisia maana na hata kubuni leksimu mpya, kunahitajika muktadha uwe ni wa kiisimu au mwingineo.

Michakato hiyo yote ya kipragragmatiki leksika inategemea zaidi muktadha. Mathalani katika mifano 28 ni muktadha unaomwezesha mtu kufanya upanuzi wa kufikia maana iii, hapo juu. Hivyo, muktadha ni kipengele muhimu katika ukuaji wa lugha na maendeleo ya kisemantiki.

Wataalamu wengi kama vile Radford et al (1999), Fromkin na Rodman (1988), Akmajian (1995), na Ullmann (1957/62), wanatoa sababu mbalimbali ambazo husababisha mabadiliko ya kisemantiki. Baadhi ya sababu hizo tumeshughulikia katika sehemu ifuatayo.

## 3.4 Sababu za mabadiliko ya kisemantiki.

Mabadiliko ya kisemantiki hutokea kwa sababu fulani, na kama anavyosema Arlotto (1972), kuna sababu mbalimbali. Kuna sababu ambazo ni za kiisimu na nyingine ambazo si za kiisimu. Katika kazi hii tumezingatia zaidi zile za kiisimu, kwa sababu ya utoshelevu wa ufafanuzi wa nadharia tumizi.

### 3.4.1 Uboreshaji maana/ uemeshaji maana

Kulingana na Tuki (1990:4), uemeshaji maana ni utaratibu unaobadili maana ya neno kuwa nzuri zaidi. Hii ni hali ambapo maana ya leksimu inapanda hadhi na kuwa bora kwa maana kwamba leksimu inapoteza maana iliyokuwa inahusishwa na hisia mbaya na kubakisha ile maana ambayo inahusishwa na hisia nzuri, Radford et al (1999), Fromkin na Rodman (1988). Kulingana na wahojiwa, leksimu ya Sheng *sota* ilikuwa inamaanisha kufilisika kabisa kimali, hivi kwamba maana hiyo ilikuwa inazua hisia mbaya. Hii leo leksimu hiyo imepoteza fahiwa ya kufilisika na kupata fahiwa ya kuishiwa na pesa ambako si lazima iwe ni hali ya kufilisika kabisa.

### 3.4.2 Udunishaji maana/ udhalilishaji maana

Katika mabadiliko ya kisemantiki leksimu huweza kuhusishwa na maana duni na hivyo watumizi lugha kususia kutumia leksimu hiyo. Hali ikitokea hivyo leksimu hiyo husemekana kudunika kimaana au kupata udhalilishaji kimaana. Katika Sheng leksimu *rasa* (kutaja leksimu *rasa* hii leo ni kama kutamka matusi fulani) inazidi kupata uduni wa kimaana na matumizi yake yanasusiwa hivi kwamba watumizi lugha hii wamekwisha buni leksimu nyingine. Badala yake wazungumzaji Sheng wamebuni leksimu *wezere* kumaanisha makalio au sehemu ya nyuma ya mtu. Uduni wa leksimu *rasa* unatokana na kuhusishwa na suruali zilizochakaa kwenye makalio na suruali kama hizo zilivaliwa na wafungwa kwenye magereza. Fahiwa hiyo haipendelewi na watumizi lugha hii na hivyo wamejitokeza na leksimu nyingine ambayo ni *wezere* kulingana na wahojiwa.

### 3.4.3 Utata

Katie (2001:15), anafafanua utata kama hali ambapo leksimu ina maana zaidi ya moja hasa katika muktadha fulani wa matumizi. Kama anavyosema Ullmann (1962:195), hali ya utata ni kigezo kikuu katika mabadiliko ya kisemantiki. Kutokana na utata leksimu huweza kufasiriwa kumaanisha vitu vingi . Kwa mfano usemi wa Sheng kama: *Wasee wako chuo*. Leksimu *chuo* ni tata kwa sababu inaweza kufasiriwa kumaanisha:

i) shule ya msingi

ii) shule ya upili

iii) chuo cha anuai

iv) chuo kikuu.

Ifahamike kwamba leksimu *chuo* ni matokeo ya ubunifu wa kileksimu unaoipa leksimu nyongeza za fahiwa hivi kwamba leksimu hii imeishia kupanuliwa kisemantiki. Kutokana na utata kama huo wa leksimu *chuo*, kumekuwepo na mabadiliko ya kisemantiki. Mabadiliko yaliyotokea mwanzoni ni yale ya leksimu *chuo* kupata fahiwa zaidi na kuishia kuwa tata inapotumika katika tungo. Ili kuondoa utata, mabadiliko mengine yametokea kwa njia ya ubunifu leksimu mpya. Leksimu zilizobuniwa ni kama zifuatazo kwa maana zifuatazo:

*i)* *Primoo-* kwa maana ya shule ya msingi.

*Wasee wa primoo ni wazii.*

Watu wa shule za msingi ni bure (Tafsiri).

i) *Sekoo-* kwa maana ya shule ya upili.

*Wasee wa sekoo ni wazii.*

Watu wa shule za upili ni bure (Tafsiri).

ii) *Kolee-* kwa maana ya chuo cha anuai.

*Wasee wa kolee ni wazii.*

Watu wa chuo cha anuai ni bure (Tafsiri).

iii) *Yunii-* kwa maana ya chuo kikuu.

*Wasee wa yunii ni wazii.*

Watu wa chuo ni bure (Tafsiri).

### 3.4.4 Unasibu wa lugha

Uhusiano baina ya leksimu na dhana zinazowasilishwa na leksimu hiyo huwa ni uhusiano nasibu. Kwa sababu hiyo maana za leksimu zina uhuru wa kubadilikabadilika baada ya muda fulani. Kama ilivyo katika lugha kwamba leksimu hubadilika, maana vilevile hubadilika kutokana na unasibu uliopo baina ya kiashiria na kiashiriwa, Saussure (1916:10). Kuchukulia lugha kama mfumo wenye komponenti zilizo nasibu kunawezesha komponeti za lugha kutazamwa kama vitu vilivyo huru na ambavyo vinaweza kubadilika. Katika misingi hiyo kiashiria kinaweza kubadilika na kiashiriwa pia kinaweza kubadilika kwa sababu mbalimbali bila kuzuiliwa na uhusiano uliopo baina yao (leksimu huweza kubadilika na maana zao vilevile). Mathalani hakuna uhusiano wa moja kwa moja baina ya leksimu *buda* (baba) na dhana *BUDA*, hivyo *buda* inaweza kutumika wakati mwingine kumaanisha kijana mwenza ambaye hata si baba ya mtu. Maana mpya ibuka zinasababishwa na uhusiano nasibu uliopo baina ya leksimu *buda* na dhana *BUDA*. Hali kama hiyo husababisha upanuzi wa kileksika.

## 3.5 Hitimisho

Katika sura hii maendeleo ya kisemantiki yamejitokeza kwa njia mbalimbali. Kwanza mabadiliko ya kisemantiki ni kigezo cha maendeleo ya kisemantiki. Pili ubunifu wa kileksimu ni ishara ya maendeleo ya kisemantiki. Kwamba kila leksimu inapobuniwa na kuingia katika lugha huwa lugha imepiga hatua ya kisemantiki hasa leksimu hiyo inapoingiza dhana nyingine katika lugha au inaposaidia kuondoa utata. Vivyo hivyo leksimu inapopata nyongeza za fahiwa na kuishia kuwa na sifa ya utata, huwa kunabuniwa leksimu mpya ili kusuluhisha utata huo. Muktadha pia umejitokeza kama kipengele muhimu katika maendeleo ya kisemantiki. Utata ni mfumo wa kisemantiki unaohusishwa na leksimu nyingi za Sheng.

SURA YA NNE

# 4.0 UBUNIFU WA KILEKSIMU NA UFASIRI WA NADHARIA YA PRAGMATIKI LEKSIKA.

## 4.0 Utangulizi

Katika sura hii tumeshughulikia ubunifu wa kileksimu, na wakati huo huo kuchanganua jinsi nadharia ya pragmatiki leksika inavyoweza kufafanua ubunifu wa kileksimu. Kulingana na Kate (2003:113), ubunifu wa kileksimu ni pale ambapo leksimu mpya inapobuniwa katika lugha au pale ambapo leksimu zilizoko katika lugha zinapopata fahiwa mpya. Tumeshughulikia ubunifu kuwili; kwanza, tumezungumzia ubunifu leksimu kama inavyojitokeza kwa leksimu mpya kubuniwa. Pili, ubunifu wa kileksimu kama inavyojitokeza kwa leksimu kupata fahiwa mpya. Mifano tuliyotoa ni ya leksimu tuliyokusanya nyanjani kutumia hojaji na mahojiano.

## 4.1 Ubunifu wa kileksimu: Ubunifu wa leksimu mpya

Huu ni mchakato ambao unachukuliwa kama aina ya upanuzi wa kileksika katika nadharia ya pragmatiki leksika. Mchakato huu huchochewa na mabadiliko ya kimuktadha kwa mujibu wa nadharia tumizi. Miktadha inaweza ikawa ya kiisimu au isiyo ya kiisimu (tazama 3.3.2). Lugha ya Sheng imepitikiwa na mfanyiko huu, labda kutokana na mfanyiko huu ndipo lugha hii inasemekana na watu kama Shitemi (2002), kuendelea kileksimu. Lugha ya Sheng hubuni leksimu hata pale ambapo kuna leksimu zenye kusimba maana za dhana hizo. Hata hivyo ubunifu huo huchochewa na masuala tata ya pragmatiki leksika kama vile mabadiliko ya kimuktadha yanayopelekea leksimu zilizoko kupata nyongeza za fahiwa au kupunguza

fahiwa. Vilevile leksimu mpya hubuniwa kusimba dhana fulani fulani ambazo ama ni mpya au zinatofautiana kimaana na leksimu za awali zilizosimba dhana hizo (mhojiwa #05).

Kila leksimu inapobuniwa huwa lugha inapokea leksimu hiyo pamoja na maana yake, hivyo kuna maendeleo ya kisemantiki ambayo huweza kudhihirika. Ubunifu wa kileksimu si jambo la kufanyika kiholela, bali ubunifu huo huenda hatua kwa hatua, kama asemavyo Arlotto (1972:170), huku akizungumzia mabadiliko ya kisemantiki. Mambo haya katika jamii lugha ni mambo ambayo hayatokei kisadfa tu. Ni mifanyiko ya kiisimu ambayo hupitia taratibu za hatua kwa hatua kupitia mkondo wa uhusishaji wa maana mbalimbali. Mifano ya maendeleo ya kisemantiki kupitia ubunifu wa leksimu mpya katika Sheng ni kama hii ifuatayo, **mfano 29**. (Data hii imewasilisha hatua kwa hatua ya ubunifu wa leksimu kama ilivyotolewa na wahojiwa.)

*dishi - mdemo.*

*chapaa- chums – doo – ganji.*

*mozo- fegi- fwaka.*

*poonyi- pai- karau- koopa- gava.*

Kulingana na utafiti wa nyanjani, awali dhana ya pesa ilisimbwa katika neno; *chapaa.* Baada ya muda leksimu hiyo ikabadilika na kuishia kutojumlisha pesa za aina ya sarafu, watumizi lugha wakajitokeza na leksimu *chums* ambayo ilitokana na ile dhana ya chuma katika Kiswahili. Dhana ya 'PESA' kuwasilishwa na leksimu *chuma* pia ikawa ni finyu na hivyo kuwacha nje pesa za aina ya noti. Watumizi Sheng wakaishia kutumia leksimu *doo*. Kutokana na dhana kwamba *doo* ina fahiwa ya pesa lakini haijasimba dhana ya uwezekano wa mtu kuwa na pesa bila kuwa na pesa taslimu, watumizi lugha hii wakabuni leksimu *ganji.* Mfumo unaojitokeza ni kuwa kila wakati kunapoongezeka dhana fulani katika hali ya matumizi,

leksimu iliyokuwa inatumika inakosa utoshelevu kisemantiki na hivyo kunabuniwa leksimu nyingine. Labda kutokana na ubunifu huu ndipo wataalamu kama Mukhwana (2008) wameishia kudai kwamba Sheng ni lugha badilifu mno. **Mifano 30.**

*chik- dem – Kenge – manzi - mshii*

*moti – buu – dinga - ndai- murenga.*

Tukichukulia dhana ya 'GARI' kuna mengi ambayo yanaweza kusemwa kuhusu ubunifu wa kileksimu katika kusimba dhana hiyo. *Motii* ni leksimu yenye maana ya kijumla sana. Kwamba ni leksimu inayosimamia gari la aina yoyote. *Buu* ni leksimu mkopo kumaanisha gari aina ya basi. Leksimu hiyo imewacha nje aina nyinginezo ya magari hasa yale madogo madogo. Kwa sababu hiyo leksimu *dinga* ilibuniwa. *Dinga* ni leksimu mwafaka zaidi na inaweza kutumika kumaanisha gari ya aina yoyote na hivyo *ndai* ni sinonimu yake. Kuna leksimu nyingine ambayo pia imeingia katika Sheng hivi karibuni, nayo ni *murenga.* Hata hivyo, kulingana na utafiti wa nyanjani leksimu hii inasusiwa kwa sababu inatokana na tabia ya matatu ya mijini ya kukwepa kutumia barabara ipasavyo na hivyo kujilazimisha kupitia kandokando ya barabara. Hadi hapo kuna dhana muhimu sana katika ubunifu huo, nayo ni muktadha. Muktadha ni dhana muhimu katika pragmatiki leksika. Aidha kipengele cha muktadha ni kichocheo kikuu katika ubunifu wa kileksimu. Hii inatokana na kwamba maendeleo ya kisemantiki hutokea katika muktadha fulani. Katika sehemu ifuatayo tumetoa mifano zaidi ya ubunifu leksimu mpya pamoja na matokeo ya utafiti wetu kuhusu ubunifu kwenye jedwali.

**Jedwali 1: Ubunifu wa leksimu mpya**

| Majibu | Frikwenzi | Asilimia |
|---|---|---|
| Ndio | 24 | 80 |
| La | 6 | 20 |
| Jumla | 30 | 100 |

Mifano ya ubunifu wa leksimu mpya kihatua kulingana na wahojiwa. (**mf 31**)

1. *Fadhee – mbuyu – buda* (baba)

Kulingana na wahojiwa, neno la awali kabisa kutumika kwa maana ya baba ni *fadhee*. Baada ya muda watumizi wa Sheng walibuni leksimu *mbuyu* na baadaye leksimu *buda*. Sababu wanazotoa watumizi kwa mkondo huo wa ubunifu wa kileksimu ni kuwa habari nyongeza inapohusishwa na leksimu, ama leksimu hiyo itabidi isheheni fahiwa hizo au leksimu nyingine ibuniwe. Leksimu inapoonekana kuwa pungufu pia leksimu nyingine hubuniwa ili kuziba upungufu huo. Sababu inayochangia leksimu kuonekana kuwa pungufu kulingana na wahojiwa ni kwamba leksimu mkopo inapobeba maana zao kutoka lugha chagizi na mara hiyo hiyo kukosa kupokezwa sifa ya upolisemia au kupanuliwa kisemantiki. Ifahamike pia kwamba wahojiwa wengine walitoa sababu za ubunifu wa kileksimu zilizo na miegemeo katika isimujamii. Kimsingi, mabadiliko ya kidhana huchangia ubunifu wa kileksimu. Mifano zaidi ya ubunifu kihatua ni kama ifutayo:

**Mifano 32**

2. *Ngoma – hewa* (muziki)

3. *Poonyi- pai- karao – koopa - gava* (polisi)

4. *Chiki – demu – kenge – manzi – mshii* (msichana)

5. *Ashara – Ashuu – kinde* (shilingi kumi)

6. *Madhee – masa – mudhama* (mama)

7. *Ushaago – shaake – shags - ocha* (sehemu ya mashambani)

8. *Rasa – wezere* (matako)

9. *Chums – ndoo – chapaa - ganji* (pesa)

10. *Mozo- fegi- fwaka* (sigara)

11. *Motii- buu- dinga- ndai- mrenga* (gari)

12. *Wahi- samba-sambare* (piga mtu)

13. *Bluu- mbao* (shilingi ishirini)

14. *Dooro- tuna- doz* (lala)

15. *Tichee- odijo- modee* (mwalimu)

Kutokana na mifano hiyo ubunifu wa leksimu mpya unajitokeza katika viwango na awamu mbalimbali. Hapo juu ubunifu wa leksimu mpya umejitokeza kama kipengee cha maendeleo ya kisemantiki kulingana na wahojiwa. Kila leksimu inapobuniwa leksimu mpya hubeba fahiwa zaidi ya leksimu ya awali. Jambo hili husababishwa na nyongeza ya kidhana kwenye akili ya watumizi lugha hii. Katika sehemu ifuatayo tunazungumzia ubunifu unavyojitokeza katika hali ya leksimu kupata fahiwa mpya. Tunarejelea maoni ya wahojiwa na mifano ya leksimu iliyotolewa na wahojiwa.

### 4.2 Ubunifu wa kileksimu: Leksimu kupata fahiwa mpya

Kama tulivyokwisha arifu, ubunifu leksimu hutokea hata pale ambapo leksimu ambazo zimekuwepo katika lugha zinapopata fahiwa mpya. Hali hii hutokea pale ambapo leksimu

fulani inapobuniwa na kisha leksimu hiyo inapoanza kuhusishwa na fahiwa zaidi. Kulingana na wazungumzaji tuliowahoji mifanyiko hii inajitokeza katika leksimu nyingi za Sheng. Ifuatayo ni mifano ya leksimu iliyopata nyongeza za fahiwa baada ya muda fulani.

**Mifano 33**

a) *Chiki* leksimu hii ilipobuniwa ilikuwa na fahiwa ya `mpenzi wa kike.' Hata hivyo baada ya muda watumizi lugha hii wakaanza kutumia leksimu hii kwa maana ya mtu yeyote mwenye jinsia ya kike.

*Mfano i): Buda ana chiki mpoa.*

Tafsiri: Baba ana mpenzi mzuri. (maana ya awali)

*Mifano ii): Machiki ni masofti vigwan.*

Tafsiri: Wasichana ni wapole sana. (maana nyongeza)

b) *Karao* ni leksimu nyingine ambayo imekuja kupokezwa fahiwa mpya. Kulingana na wazungumzaji lugha hii, leksimu hii ilibuniwa kumaanisha polisi wa kuzima ghasia hasa miongoni mwa wanafunzi wa chuo wanapoandamana au wanapogoma.

*Mfano i) : Msee kuna makarao kwa chuo.*

Tafsiri : Jamaa, kuna polisi chuoni.

*Mfano ii) wakorino hutuna kwa baro.*

Tafsiri: Polisi wa trafiki huzubaa barabarani.

Leksimu *makarao* katika mfano i ina maana ya polisi wa kuzima ghasia ilhali mfano ii ina fahiwa ya polisi wa trafiki ambao kazi yao hukita kwenye barabara.

c) *Wahi.* Awali leksimu hii ilikuwa inatumiwa kumaanisha kumpiga mtu. Kutokana na matumizi yaliyopanuliwa leksimu hii ikajakupata fahiwa zaidi. Hii leo leksimu hii ina maana zaidi kama vile kumpiku mtu katika kutenda jambo, kugundua ujanja wa mtu fulani. Fahiwa nyingine ya leksimu hii ni kufanikiwa kutongoza msichana.

*Mfano i) Nimemwahi msee fulani.*

Tafsiri: Nimempiku mtu fulani.

*Mfani ii) Nimewahi mshii msupu.*

Tafsiri: Nimefanikiwa kutongoza msichana mrembo.

d) *Sorora.* Kulingana na wahojiwa, hiki ni kitenzi ambacho kimepata fahiwa nyongeza. Leksimu hii mwanzo ilimaanisha kuangalia mtu kutumia macho. Fahiwa nyongeza hii leo ni kufanya ujasusi au upekuzi, na siyo upekuzi tu bali ni upekuzi unaofanywa na polisi. Hivyo *msororaji* ni mtu anayefanya kazi ya ujasusi au upekuzi. Wakati mwingine pia leksimu *msoroo* hutumika.

*Mifano: Magava wasoroo wamekamu.*

Tafsiri: Polisi wapekuzi wamekuja.

e) *Tuna* ni leksimu ambayo maana yake ilikuwa ni kulala. Hata hivyo leksimu hii imepokezwa maana nyingine ambayo ni kuzubaa.

*Mfano i) Mkidi ametuna kwa mbanyu.*

Tafsiri: Mtoto amelala kwa nyumba.

*Mfano ii) Magava hutuna baro.*

Tafsiri: Polisi wa trafiki huzubaa kwa barabara.

Kutokana na leksimu za Sheng kuzidi kupokezwa fahiwa mpya, leksimu nyingi zimeishia kuwa na sifa ya upolisemia. Katika sehemu ifuatayo upolisemia umeshughulikiwa kwa kutoa mifano ya Sheng.

### 4.3 Upolisemia

Leksimu nyingi katika lugha huwa na maana nyingi kutokana na leksimu kuzidi kupokezwa fahiwa nyongeza na watumizi lugha. Maana nyongeza huwa za pembeni mwanzo mwanzo wa matumizi, hata hivyo baada ya muda maana za pembeni huweza kuchukua nafasi za maana kuu kama wasemavyo Radford et al (1999). Mifanyiko hiyo husababisha ubunifu wa kileksimu wa nyongeza za fahiwa mpya kwa leksimu husika. Wakati maana ya pembeni inapokuwa maana kuu si lazima leksimu hiyo ipoteze maana za awali. Leksimu katika lugha huweza kupoteza maana na vilevile huweza kupata maana zaidi. Msisitizo katika sehemu hii ni leksimu kupata fahiwa mpya. Leksimu inapopata maana zaidi bila kupoteza ile ya awali huwa leksimu hiyo inapata sifa ya upolisemia.

Upolisemia ni tofauti na utata ( tazama 3.4.3). Kimsingi upolisemia ni hali ambayo leksimu moja ina maana nyingi na leksimu hiyo huwa ni moja tu katika orodha ya leksimu kwenye kamusi za lugha husika. Upolisemia ni hali ya leksimu moja kuwa na maana nyingi zenye ukaribu. Leksimu *wahi* katika Sheng ina fahiwa nyingi, kama vile: **Mifano 34**

i. Kumshinda mtu katika kutenda jambo.

Mfano. *Nimemwahi modee.*

Nimemshinda mwalimu (tafsiri).

ii. Kumpiga mtu.

Mfano. *Nimemwahi vinoma.*

Nimempiga vibaya (tafsiri).

iii. Kugundua ujanja wa mtu.

Mifano. *Nimewahi njaro zake.*

Nimegundua ujanja wake (tafsiri).

Leksimu *wahi* kama zilivyo leksimu nyingi katika Sheng ina sifa ya upolisemia. Upolisemia ni mfumo wa kisemantiki unaohusisha fahiwa nyingi na leksimu moja katika lugha. Ikumbukwe kwamba leksimu inapopata nyongeza za fahiwa, pamoja na kwamba leksimu hiyo huishia kupata sifa ya upolisemia pia mfanyiko huo huchukuliwa kama ubunifu wa kileksimu chini ya upanuzi wa kileksika katika nadharia ya pragmatiki leksika.

### 4.4 Maoni ya wahojiwa kuhusu ubunifu wa kileksimu na sababu za ubunifu huo

Tunakumbusha hapa kwamba ubunifu wa kileksimu umetumika hapa kama mchakato wa upanuzi wa kileksimu katika nadharia ya pragmatiki leksika. Hivyo ubunifu hutokea pale ambapo leksimu mpya inabuniwa na hata leksimu zilizoko katika lugha kupata nyongeza za kifahiwa.

Asilimia 82.3 ya wahojiwa wanashikilia kwamba ubunifu wa kileksimu husababishwa na mazingira. Kwamba mazingira tofauti huzalisha leksimu tofauti tofauti kwa maana fulani fulani. Aidha maendeleo ya kiteknolojia katika jamii pia ni mojawapo ya sababu ya ubunifu

wa kileksimu. Kwa sababu ya maendeleo hayo dhana fulani huingizwa katika jamii na jamii lugha hubuni leksimu ya kusimba au kusetiri maana hiyo. Mabadiliko hayo pia kulingana na wahojiwa husababisha leksimu zilizoko kupunguza fahiwa au fahiwa zilizoko kuwa hafifu na hivyo kuchangia ubunifu wa leksimu nyingine. Kwa mfano mhojiwa #6 anasema kwamba shilingi ishirini ilipatiwa leksimu *bluu* kwa sababu hapo awali shilingi ishirini ilikuwa ni noti yenye rangi ya bluu; baadaye noti hiyo ilitoweka kutokana na sera za benki kuu ya Kenya. Hivyo shilingi ishirini ikawa sarafu. Kutokana na mabadiliko hayo watumizi Sheng wakabuni leksimu *mbao* kwa maana hiyo hiyo. Leksimu pia huenda ikapata nyongeza ya fahiwa, mifano ni leksimu *chizi* ambayo hapo awali ilimaanisha mwendawazimu; hii leo leksimu hiyo imepata nyongeza ya fahiwa na sasa maana yake nyingine ni mtu asiyekuwa na mpangilio katika mambo yake, yaani yule aliyechanganyikiwa.

Wahojiwa asilimia 87.3 pia wanaonelea kuwa ubunifu wa kileksimu unatokea kwa ajili ya leksimu kuwa na ukaribu wa kimaana. Hivyo ili kubaini kwa hakika dhana fulani kutoka kwa nyingine leksimu mpya hubuniwa. Watumizi Sheng wanahoji kwamba lugha ya binadamu ni badilifu kama binadamu mwenyewe hivyo lazima leksimu nazo zibadilike kuakisi mabadiliko ya binadamu. Kwa sababu hiyo, leksimu nyingi hubuniwa kila mara na leksimu zilizoko kupata fahiwa zaidi; hali kadhalika nyingine kupunguza fahiwa.

Kulingana na wahojiwa asilimia (86.7) wanaonelea kuwa ubunifu wa kileksimu hutokea katika Sheng. Aidha wahojiwa wanaonelea kuwa ubunifu wa kileksimu ni njia mojawapo ya maendeleo ya kisemantiki. Wengi wanaonelea kuwa leksimu inapobuniwa huwa na maana fulani na husimba dhana fulani katika ulimwengu wa watumizi lugha. Hivyo mfanyiko wa

ubunifu wa kileksimu ni maendeleo ya kisemantiki. Ubunifu wa kileksimu hutokea kama taratibu za kuunda leksimu kupitia mbinu ambazo zimejadiliwa katika sura ya pili, pia ni mifanyiko ya kisemantiki inayochangiwa na upanuzi wa maana katika lugha.

Kuna pale ambapo majukumu ya mtu yanapobadilika, watumizi Sheng pia hubuni leksimu ya kuakisi uhalisia huo. Mfano uliotolewa na watumizi lugha ni ule wa leksimu *tichee* ambayo ilibadilika na kuwa *odijo* na sasa ni *modee.* Kulingana na watumizi lugha hii leksimu *modee* ilibuniwa baada ya serikali ya Kenya kupiga marufuku kutumika kwa viboko katika shule za Kenya. Hivyo tofauti na ilivyokuwa hapo awali kwamba *odijo* alikuwa ni mtu mwenye kubeba kiboko cha kuwachapa wanafunzi wakorofi, sasa *modee* imesimba fahiwa ya mwalimu lakini asiyewachapa wanafunzi wakorofi bali ni mwalimu mwenye kuwashauri wakorofi kubadili tabia bila kutumia kiboko. Kifupi, jukumu la mwalimu kuwaadhibu wanafunzi kwa kutumia kiboko limebadilika na sasa mwalimu anapaswa kutoa mashauri kwa mwanafuzi mwenye makosa. Ni kutokana na mabadiliko hayo ya majukumu ndipo leksimu *modee* ilipobuniwa.

Katika utafiti huu pia tuliwahoji wazungumzaji wa lugha hii kwa njia ya ana kwa ana. Kama ilivyokuwa katika hojaji, wahojiwa wa ana kwa ana walikuwa wakazi wa Jeriko jijini Nairobi; sehemu mojawapo inayodaiwa na Osinde kuwa Sheng ilizukia. Mahojiano haya yalichukua wiki moja, malengo yakiwa ni kupata maoni ya watu kuhusu ubunifu wa kileksimu katika Sheng na maendeleo ya kisemantiki kwa ujumla. Katika mahojiano haya pia tulipata kukusanya leksimu tulizochanganua katika sura ya pili kwa misingi ya taratibu au mbinu za uundaji wao. Tuliuliza wahojiwa kutoa maana za leksimu fulani fulani pamoja na kubaini leksimu hizo kama ni vitenzi au nomino.

Wahojiwa asilimia 86.7 walikubali kwamba ubunifu wa kileksimu katika Sheng upo na ubunifu huo ni tukio linalotokea kila kuchao. Wahojiwa watatu walikiri kwamba Sheng kama lugha ina uzalishaji mkubwa sana wa leksimu hivi kwamba leksimu ni nyingi za kutajia dhana fulani moja. Hata hivyo mhojiwa mmoja alidai kuwa leksimu ambazo hudhaniwa kuwa visawe, si visawe kwa sababu leksimu hizo zinasimba fahiwa mbalimbali za dhana kuu moja. Mhojiwa huyu kwa sababu ni mwandishi wa habari alitambua kwamba leksimu fulani inapopoteza fahiwa fulani, inabidi watumizi lugha ama kubuni leksimu nyingine mpya au kuongezea fahiwa hiyo kwa leksimu iliyopo ili kufidia upungufu huo. Mhojiwa huyu alitoa mfano wa dhana BABA – ambayo alisema kwamba kwa mujibu wa watumizi wa Sheng ina leksimu nyingi lakini kila leksimu imebeba fahiwa tofauti. Kwa mujibu wa mhojiwa huyu neno ambalo anasema ni la awali kabisa ni lile la *fadhee*. *Fadhee* anasema ni leksimu yenye kubeba dhana ya jumla ya baba. Hivyo baada ya wazungumzaji kutambua ujumla huo walibuni *mbuyu*-ambayo ilisimba dhana ya baba lakini si baba tu bali ni baba ambaye ana umri wa wastani – lakini ambaye ana tabia ya ukali kwa watoto wake. *Buda* kwa upande wake, pamoja na kwamba ina fahiwa ya baba, ni baba ambaye amefika umri wa kustaafu au yuko katika umri wa uzee wake. Katika mahojiano hayo tulitambua kuwa neno *buda* linaweza kutumika katika muktadha fulani na likawa na maana ya utani, kwamba kijana mwenye jinsia ya kiume anaweza akamwita mwenzake *buda*.

Kutokana na mahojiano ya ana kwa ana imejitokeza kwamba maendeleo ya kisemantiki huweza kujitokeza kupitia ubunifu wa kileksimu. Wahojiwa asilimia 83.7 wanakiri kwamba ubunifu huo una mantiki na umesheheni mfumo wa kisemantiki. Lau kama hakungekuwepo na mfumo wowote, mawasiliano yangekuwa na matatizo mengi. Matokeo ya mahojiano pia yanaonyesha kwamba ubunifu wa kileksimu umekita katika miktadha mbalimbali. Aidha

matokeo yanaonyesha uhusiano fulani wa maana asilia na maana mpya hasa katika leksimu mkopo. Ubunifu wa kileksimu pia huweza kujitokeza kwa njia mbalimbali kulingana na wahojiwa. Mfumo wa wazi wa kisemantiki unaojitokeza ni kwamba leksimu zinapopata fahiwa nyongeza leksimu hiyo hupata sifa ya upolisemia, upolisemia unaposababisha utata wa maana ya leksimu, ubunifu wa leksimu mpya hutokea.

## 4.5 Hitimisho

Sura hii imeshughulikia ubunifu wa kileksimu kwa kurejelea zaidi maoni ya watumizi lugha hii kama yalivyojitokeza kwenye hojaji na mahojiano. Matokeo yanaonyesha kuwa kuna ubunifu wa kileksimu katika lugha ya Sheng na kwamba ubunifu wa kileksimu ni njia mojawapo ya maendeleo ya kisemantiki. Ubunifu umejitokeza kuwili, ule wa leksimu mpya na wa leksimu kupata fahiwa zaidi.

Wahojiwa wengi wanakiri kwamba ubunifu wa kileksimu katika Sheng si jambo la kiholelaholela bali ni mifanyiko ya kiisimu yenye mantiki na mfumo dhahiri wa kisemantiki. Ubunifu wa kileksimu ni mfanyiko wa juhudi za kimaksudi za watumizi Sheng. Kama ambavyo tumeona hapo awali ubunifu wa kileksimu hutokea kutokana na leksimu kupata fahiwa zaidi na kuishia kuwa na upolisemia. Upolisemia huo husababisha utata wa kimaana hasa katika matumizi hivi kwamba leksimu mpya hubuniwa kusuluhisha utata wa kimaana na muktadha vilevile husaidia kuondoa utata. Mambo haya yote yanafasiriwa chini ya nadharia ya pragmatiki leksika.

# SURA YA TANO

## 5.0 MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 5.1 Utangulizi

Utafiti huu ulinuia kushughulikia maendeleo ya kisemantiki kupitia ubunifu wa kileksimu. Aidha tulilenga kubaini mfumo wowote wa kisemantiki unaojitokeza katika maendeleo hayo na jinsi muktadha unavyochangia ubunifu wa kileksimu. Ili kufikia malengo hayo tulitumia nadharia ya pragmatiki leksika kama kifaa cha uchunguzi. Katika kutumikiza nadharia hii tulitaka kupimia utoshelevu wa kifafanuzi wa pragmatiki leksika, hasa ufafanuzi wa michakato ya ubunifu wa kileksimu kama njia ya upanuzi wa kileksika. Ili tutimize malengo yetu ilitubidi tutumie hojaji na mahojiano ya ana kwa ana ilimuradi tupate data msingi. Kazi yetu ilipangiliwa katika sura tano. Ifuatayo ni muhtasari wa sura hizo.

### 5.2 Muhtasari

Katika sura ya kwanza, tumeshughulikia vipengele vifuatavyo: Utangulizi, usuli wa mada-hapa ndipo tulirejelea asili na chimbuko la Sheng pamoja na kutathmini mijadala ya mielekeo, maoni na misimamo ya wataalamu mbalimbali kuhusu Sheng; tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, nadharia tete, sababu za kuchagua mada hii, upeo na mipaka ya utafiti, misingi ya kinadharia, njia za utafiti na mwishowe umuhimu wa utafiti.

Katika sura ya pili tumezungumzia mbinu za uundaji leksimu. Mbinu zimejadiliwa kama michakato bia yenye kutumika na lugha yoyote ulimwenguni. Japo tumefanya hivyo ilijitokeza kwamba mbinu fulani fulani zina uzalishaji kuliko nyingine katika lugha ya Sheng. Mbinu tulizozungumzia ni pamoja na: Ukopaji na utohozi, ubunifu, ukatizaji, uambishaji, ubadilishaji silabi, onomatopea, ujenzi ghairi, akronimu, kaleki, uhulutishaji, taratibu

changamano, uambatishaji, upolisemia, unyumbuzi kapa na ubadilishaji rajamu kuwa maneno kamili. Baadhi ya mbinu hizo ndizo hutumika katika ubunifu wa kileksimu.

Katika sura ya tatu tumezungumzia maendeleo ya kisemantiki na ufasiri wa nadharia ya pragmatiki leksika. Katika kufanya hivyo tumezungumzia mabadiliko ya kisemantiki yanayokumba leksimu za Sheng. Baadhi ya mabadiliko yaliyoshughulikiwa ni kama vile: Upanuzi, ubanifu wa kileksika, matumizi ya kitamathali, na ukisivu wa maana. Mabadiliko haya baadaye yalijadiliwa kama michakato ya nadharia ya pragmatiki leksika. Hali kadhalika tulitambua umuhimu wa muktadha katika nadharia ya pragmatiki leksika na hivyo tukauzungumzia pia. Tumemaliza sura hii kwa kujadili sababu zinazochangia mabadiliko ya kisemantiki. Sababu zenyewe ni kama vile: Uboreshaji maana, udunishaji maana, utata, na unasibu wa lugha. Nadharia tumizi ilitumika kupata istilahi za ufafanuzi.

Katika sura ya nne tumezungumzia ubunifu wa kileksimu na ufasiri wa nadharia ya pragmatiki leksika. Tumezungumzia ubunifu wa leksimu mpya na ubunifu unaotokea kwa leksimu kupata fahiwa mpya. Tumeshughulikia upolisemia kama matokeo ya leksimu kupata fahiwa zaidi na kumalizia kwa maoni ya kijumla ya wahojiwa. Kutokana na utafiti wetu tumejitokeza na hitimisho kama ifuatavyo:

### 5.3 Hitimisho

Imejitokeza kwamba lugha ya Sheng ina taratibu za kuunda leksimu zake kama zilivyo lugha za kilimwengu. Leksimu zilizoundwa husimba dhana fulani fulani katika ulimwengu wa watumizi lugha hii. Baada ya muda fulani leksimu zilizoundwa hubadili maana. Kubadilika kwa maana hudhihirisha maendeleo ya kisemantiki. Imekuwa wazi kwamba leksimu

zinapochukua maana za kijumla kunabuniwa leksimu nyingine ili kuafiki maana hiyo mahsusi iliyotengwa wakati leksimu ilipochukuwa maana ya jumla. Aidha imejitokeza pia kuwa leksimu inapokuwa hafifu kimaana leksimu nyingine hubuniwa ili kufidia maana hiyo. Leksimu inapopata nyongeza ya maana huweza kupanuka kimaana au leksimu badala kubuniwa. Kimsingi ubunifu wa kileksimu umejitokeza kuwili; kwanza, ubunifu wa leksimu mpya na leksimu kupata fahiwa mpya. Kwa sababu hizo haipothesia yetu ya kwanza iliyodai kwamba ubunifu wa kileksimu katika lugha ya Sheng inadhihirisha maendeleo ya kisemantiki ni haipothesia ya kweli. Hii ni kwa sababu kunapobuniwa leksimu huwa kuna nyongeza ya kidhana katika lugha na hayo ni maendeleo ya kisemantiki, hivyo tukafikia lengo letu la kwanza.

Jambo la pili ambalo limejitokeza kupitia utafiti huu ni kwamba muktadha ni kipengele chenye kusababisha ubunifu wa kileksimu; leksimu zilizoko katika lugha kupata nyongeza za fahiwa au leksimu mpya kubuniwa. Wakati mwingine pia kuna hali ya kupunguka kwa fahiwa. Mabadiliko katika muktadha halisi na muktadha dhahania huchangia pakubwa kubuniwa kwa leksimu. Imejitokeza kwamba mabadiliko ya kiteknolojia, kiuchumi, kisiasa, majukumu, na nyongeza za kidhana huchangia ubunifu wa kileksimu. Mabadiliko haya huweza kukita kwenye hali halisi ya kilimwengu au matukio ya kisaikolojia. Kutokana na tathmini yetu, haipothesia ya pili iliyodai kuwa mabadiliko ya kimuktadha huchangia ubunifu wa kileksimu au leksimu kupata nyongeza za fahiwa au upungufu wa fahiwa inakubalika kuwa ya kweli na kutimiza lengo letu la pili. Taratibu ya ubunifu wa kileksimu ni michakato ya pragmatiki leksika chini ya mfanyiko wa upanuzi.

## 5.4 Mapendekezo

Katika utafiti huu tulipitia changamoto nyingi zikiwemo ukosefu wa fedha za kutosha, ufinyu wa muda na usumbufu kutoka kwa wahojiwa. Hata hivyo tulifanikiwa kukamilisha utafiti wetu. Katika utafiti huu tulibanwa kwa upeo na mipaka yetu na hivyo tulichanganua maendeleo ya kisemantiki kupitia ubunifu wa kileksimu. Tulifanya hivyo kwa kukita katika nadharia ya pragmatiki leksika. Japo utafiti huu umeshughulikia ubunifu wa kileksimu kama njia mojawapo ya maendeleo ya kisemantiki, bado utafiti zaidi unahitajika hasa kwa kutumikiza michakato mingineyo ya pragmatiki leksika. Kwa sababu hiyo tumependekeza utafiti zaidi juu ya mambo yafuatayo:

1. Utafiti zaidi ufanywe kuhusu uzuiliaji wa kileksika katika leksimu za Sheng.
2. Utafiti zaidi ufanywe kuhusu jinsi ya usimbaji maana za tamathali za usemi za Sheng na jinsi mifanyiko hiyo inavyoathiri semantiki ya lugha hii na inavyochangia ubunifu wa kileksimu katika lugha hii.
3. Katika uchunguzi huu tuligundua kwamba upolisemia unatokea baina ya lugha mbili. Kwamba leksimu ikikopwa, katika lugha pokezi leksimu hiyo hupanuliwa kisemantiki. Uchunguzi zaidi unahitajika kutathmini kama nadharia ya pragmatiki leksika inaweza kufafanua mifanyiko hiyo.

**Baadhi ya istilahi muhimu katika kazi hii**

| | |
|---|---|
| Akronimu | - *Acronymy* |
| Dhana za kidharura | - *Ad hoc concepts* |
| Isimujamii | - *Sociolingustics* |
| Jinsia | - *Gender* |
| Jumuiya lugha | - *Speech Community* |
| Kirioli | - *Creole* |
| Kufululiza kwa lugha | - *Language continuum* |
| Lahaja | - *Dialect* |
| Leksimu | - *Lexeme* |
| Leksikoni | - *Lexicon* |
| Lingua franka | - *Lingua franca* |
| Lugha mchanganyiko | - *Mixed language* |
| Msimbo | - *Code* |
| Onomatopea | - *Onomatopeia* |
| Pijini | - *Pidgin* |
| Pragmatiki leksika | - *Lexical pragmatics* |
| Sajili | - *Register* |

| | |
|---|---|
| Sera ya lugha | - *Language policy* |
| Semantiki leksika | - *Lexical semantics* |
| Tafsiri kopa/ kaleki | - *Loan translation/ calque* |
| Mabadiliko ya kisemantiki | - *Semantic change* |
| Muktadha | - *Context* |
| Maendeleo ya kisemantiki | - *Semantic development* |
| Uambatishaji | - *Compounding* |
| Uambishaji | - *Affixation* |
| Ubadilishaji msimbo | - *Code switching* |
| Ubadilishaji silabi | - *Sylable reversing* |
| Ubanifu | - *Narrowing* |
| Uboreshaji maana | - *Amelioration* |
| Ubunifu | - *Coinage* |
| Ubunifu wa kileksimu | - *Neologism* |
| Uchanganyishaji msimbo | - *Code mixing* |
| Udunishaji maana | - *Perjoration* |
| Ujenzi ghairi | - *Back formation* |
| Uhawilishaji | - *Adaptation* |

| | |
|---|---|
| Uhulutishaji | - *Blending* |
| Ukatizaji | - *Clipping* |
| Ukisivu maana | - *Approximation* |
| Ukopaji na utohozi | - *Borrowing and adaptation* |
| Unasibu | - *Abittrariness* |
| Upanuzi | - *Broadening* |
| Upangaji lugha | - *Language planning* |
| Upanuzi wa kileksika | - *Lexical broadening* |
| Upanuzi wa kikategoria | - *Category extension* |
| Upanuzi wa kisemantiki | - *Semantic expansion* |
| Upolisemia | - *Polysemy* |
| Unyumbuzi kapa | - *Zero derivation* |
| Wingilugha | - *Multilingualism* |

## MAREJELEO


Abdulaziz, M. na Osinde, K. (1997) Sheng and Engsh in Nairobi: Development of mixed codes among the urban youth in Kenya. *International Journal of the Sociology of Language,125: 43*-63

Adams, V. (1973) *An Introduction to Modern English word formation*. London: Longman.

Aitchison, J. (2002) *Language Change: Progress or Decay? Third edition*. Cambridge: Cambridge University Press.

Aitchison, J. (2002) *Words in the Mind: An Introduction to Mental Lexicon Third Edition.* U.S.A: Blackwell Publishers Ltd.

Akmajian et al (2001) *Linguistics: An Introduction to Language and Communication* (*Fifth Edition)*. Cambridge: MIT.

Arlotto, A. (1972) *Introduction to Historical Linguistics*. New York: Houghton Mifflin Company.

Barsalou, L. (1987) The Instability of graded structure: Implications for nature of concepts katika U. Neisser (mh) *Concepts and conceptual development.* Cambridge. Cambridge University Press.

Beaugrande, R na Dressler, W. (1981) *Introduction to Textlinguistics*. New York: Longman.

Blutner, R. (1998). Lexical pragmatics. *Journal of Semantics, 15*, 115-162.

Blutner, R. (2000). Some aspects of optimality in natural language interpretation. *Journal of Semantics, 17*, 189-216.

Blutner, R. (2002). Lexical semantics and pragmatics. *Linguistische Berichte, 10*, 27-58.

Blutner, R. (2004). Pragmatics and the lexicon. Katika L. Horn and G. Ward (Mh.), *Handbook of pragmatics*. Oxford: Blackwell.

Bosire, M. (2008) *Sheng*: The phonological, Morphological and Social Profile of an urban venacular. Tasnifu ya Uzamifu ambayo haijachapishwa: University of Albany, State University of New York.

Bosire, M. (2009) 'What makes a Sheng word unique? Lexical manipulation in mixed Languages.'*Selected proceedings of the 39th Annual conference on African Lingustics, somervile. MA.*

Carston, R.(2004) *Thoughts and Utterance: The Pragmatics of Explicit Communication.* Oxford: Blackwell Publishers Ltd.

Echessa, P.G. (1990) A Study of the word structure and processes involved in word formation in Sheng: A Case Study of Eastlands area in Nairobi. Tasnifu ya Uzamili ambayo bado haijachapishwa, Chuo kikuu cha Nairobi.

Fodor, J.B. (1977) *Semantics: Theory of meaning in Generative Grammar*. Cambidge: Harvard University Press.

Fromkin, V. na R. Rodman. (1988) *An Introduction to Language*. Fouth Edition. Orlando Florida: Harcourt Brace Jovanovich the Dryden press.

Githinji, P. (2003) Language Attitudes: Nairobi people and Sheng.Tasnifu ya Uzamili ambayo bado haijachapishwa, Michigan State University.

Githinji, P. (2006a) Sheng and Variation: The construction and Negotiation of layered identities. Tasnifu ya Uzamifu ambayo bado haijachapishwa, Michigan State University.

Githinji, P. (2006b) 'Bases and their shiboleths: Lexical Variation and Sheng speakers' identities in Nairobi'. *Nordic Journal of African Studies,15(4),443-472.*

Githiora, C. (2002) 'Sheng: Peer Language, Swahili dialect or emerging Creole? *Journal of African studies.15(2):159-181.*

Grice, H.P., (1989) *Studies in the Way of Words.* Cambidge, MA: Harvard University Press.

Hartmann R.R.K. & Stork F.C.(1972) *Dictionary of Language and Linguistics*. London: Applied Science Publishers Ltd.

Hock, H.H. na B.D. Joseph (1996) *Language History, Language Change and Language Relationship: An Introduction to Historical and Comparative Linguistics.* New York: Mouton de Gruyler Berlin.

Huddleston, R.et al. (2002) *The Cambridge Grammar of English Language*. UK. Cambridge.

Hudson, R.A.(1996) *Sociolinguistics*. 2nd Edition. Cambridge. C.U.P

Iribe, P.M. (1996) Matatizo ya Leksikografia Tafsiri katika kamusi ya F. Johnson 1939. Tasnifu ya Uzamili ambayo bado haijachapishwa. Nairobi. Chuo kikuu cha Nairobi.

Iribemwangi, P.I. & Mukhwana, A.(2011). *Isimujamii*. Nairobi. Focus Publishers ltd.

Karanja, L.(2010) 'Homeless' at home : Lingustic, Cultural and Identity, Hybridity and Third Space Positioning of Kenyan Urban Youth. *Education canadienne et internationale, 39(2):1-10*

Karanja, M.N. (1993) *Miaka 50 katika Jela*. Nairobi. Heinman Kenya.

Katamba, F. (1993) *Morphology.* Cambridge: Cambridge University Press.

Katie, W. (2001) *A Dictionary os Stylistics*. Longman. Harlow.

Katz, J. (1972) *Semantic Theory*. New York: Harper and Row.

Keans, K. (2000) *Semantics*. London. Palgrave.

Kembo-Sure (1992) 'The coming of Sheng'. *English Today 26-28*

Kiessling, R. na Mous, M. (2001) Urban Youth Languages in African. *Paper presented at the conference on Language, Migration and the City, November* 22-24, 2001. Bayreuth: University of Bayreuth.

King'ei, K. (2001) Language and identity: The challenge of Sheng in Kenya. *Paper presented at the Association of Third World studies conference, September* 17-19, 2001. Njoro, Egerton University, Kenya.

Lascardes, A. et al (1996) Ambiguity and Coherence. *Journal of Semantics 13: 41-65.*

Lasersohn, P. (1999) Pragmatics halos. *Language* 75: 22-555

Lewis, D. (1983) Philosophical.Oxford: Oxford University Press

Lipka, L.(1990) *An Outline of English Lexicology; Lexical Structure, Word Semantics and Word Formation.* Tuebingen:Max Niemeyer.

Palmer, F.R (1981) *Semantics. Second Edition*. Cambridge: Cambridge University Press.

Lyons, J. (1977) *Semantics.* Cambridge. Cambridge University Press.

Makokha, W.O.(2010). Uchanganuzi wa kiisimu wa baadhi ya matini za Kiswahili: Mtazamo wa Pragmatiki Leksika. Nairobi. Chuo kikuu cha Nairobi, Tasnifu ya uzamili ambayo bado haijachapishwa.

Matthews, P.H. (1997) *A concise Dictionary of Linguistics*. New York. Oxford University Press.

Mazrui, A.M.(1995) 'Slang and code-switching: The case of sheng in Kenya.'*Afrikanistische Arbeitspapier 42:168-179.*

Mazrui, A.M na Mphande, L.(1990)' How is a code mixer's grammar organized?' Evidence from Sheng. *Paper presented at the 21st Annual conference on African Linguistics*, April 12-14, 1990

Mbaabu, I. na Nzuga, K (2003) *Sheng-English Dictionary: Deciphering East Africa's Underworld Language*. Dar es Salaam: TUKI.

Moga, J. na Fee, D.(1993*) Sheng Dictionary*. Nairobi: Ginsen Publishers.

Momanyi, C. (2009) The effect of 'Sheng' in the teaching of Kiswahili in Kenyan schools.*The Journal of Pan African Studies, 12:127-138*

Mgullu, R.S (1999) Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili. Nairobi: Longhorn Publishers.

Munga, G.M.(2009). Sense Relations in Gikuyu: A lexical Pragmatics Approach. Nairobi. Chuo kikuu cha Nairobi, Tasnifu ya uzamili ambayo bado haijachapishwa.

Mukhwana, A (2008) Language Attitudes in Nairobi, Mombasa and Kisumu. Tasnifu ya Uzamifu ambayo bado haijachapishwa.

Ngesa, M.(2002) And Sheng lives on..........*Profile. East African Standard 16-22 Feb, 2001.*

Obuchi, S.M. na A. Mukhwana. (2010) *Muundo wa Kiswahili: Ngazi na Vipengele*. Nairobi: Aframe publishers.

Ogechi, N.O.(2002) Trilingual Codeswitching in Kenya-Evidence from Ekegusi, Kiswahili, English and Sheng. Tasnifu ya Uzamifu ambayo haijachapishwa. Hamburg: University of Hamberg.

Ogechi, N.O. (2005) On Lexicolization in Sheng. *Nordic Journal of African Studies. 14(3),334-355*

Osinde, K.(1986) Sheng; an Investigation into the Social and Structural Aspects of an Evolving Language. Tasnifu ya BA ambayo bado haijachapishwa. Nairobo: Chuo kikuu cha Nairobi.

Pyles, T. na J. Algeo (1982) *The Origins and Development of English Language*. Third Edition. New York: Harcourt Brace Jovanovich publishers.

Quirk, R.et al (1973) *A University Grammar of English*. London. Longman.

Radford, A. Etal (1999) *Linguistics: An Introduction*. Cambridge: Cambridge University Press.

Richards et al (1985) *Longman Dictionary of Applied Linguistics*. UK. Longman Group.

Samper, H.(2002) Taking sheng: The role of a hybrid language in the construction of identity in youth culture in Nairobi, Kenya. Tasnifu ya Uzamifu ambayo bado haijachapishwa. University of Pennsylvania

Saussure, F.(1916) *Course in General Linguistics*. London: Duckworth.

Shitemi, N.L. (2002) Pidginization: Sheng, the melting- pot of the Kenyan Language and an anti-Babel development. *Kiswahili 64:1-15*

Singleton, D. (2000) *Language and the Lexicon: An Introduction.* New York: Oxford University Press.

Sperber, D. na Wilson, D. (1995) *Relevance: Communication and Cognition Second Edition.* Oxford: Blackwell Publishers Ltd.

Sperber, D. na Wilson, D. (2002) Pragmatics, modularity and mindreading. *Mind & Language* 17: 3-23.

Spyropoulos, M. (1987) Sheng: Some preliminary investigation into a recently emerged Nairobi street language. *Journal of the anthropological Society of Oxford, 18(18):125-136*

Trask, (1994) *Language Change.*London na New York: Routledge.

Trudgill, P. (1974) *Sociolingustics*: *An introduction to Language and Society*. England: Penguine books. Ullmann, S. (1957) *The Principles of Semantics*. Great Britain: Blackwell and Mott.

Ullmann, S. (1962) *Semantics. An Introduction to Science of Meaning*. Great Britain: Blackwell and Mott.

Waithira, C.(2001) A study of the Structure of the youth jargon in Nairobi. Tasnifu ya uzamili ambayo bado haijachapishwa.

Wambugu, M.W.(2010). Semantic Shifts in Gikuyu Lexemes: A Lexical Pragmatics approach. Nairobi. Chuo kikuu cha Nairobi, Tasnifu ya uzamili ambayo bado haijachapishwa.

Widdowson, H.G.(1996). *Linguistics.*United Kingdom. Oxford University Press.

Wilson, D. na D. Sperber. (2002) Truthfulness and Relevance.*Mind.* 111.3-6

Wilson, D na D. Sperber. (2004) Relevance Theory katika L. Horn na G. Ward (Mh). *The Handbook of Pragmatics.* Blackwell: Oxford University Press.

Yule, G. (1985) *The Study of Language*. Cambridge. Cambridge University PressUzamili ambayo bado haijachapishwa. Eldoret. Chuo kikuu cha Moi.

**KIAMBATISHO A**

**HOJAJI**

*Mimi ni mwanafunzi wa somo la isimu ya Kiswahili( uzamili) katika chuo kikuu cha Nairobi. Nafanya utafiti juu ya Sheng. Naomba uchukue muda wako kunijazia hojaji hii. Toa habari za kweli bila uwoga wowote na usiandike jina lako popote. Habari zote zitashughulikiwa kama siri.*

**Sehemu A ( tia alama kwa chaguo lako)**

1. Umri wako unapatikana katika kategoria gani?
    a) 14- 20
    b) 21- 25
    c) 26- 35
    d) 36- 45
    e) 46 na zaidi
2. Jinsia
    a) Uume
    b) Uuke
3. Kiwango chako cha elimu.

a) Elimu ya shule ya msingi

b) Elimu ya shule ya upili

c) Elimu ya chuo cha anuai

d) Elimu ya chuo kikuu

e) Nyingineyo bainisha.......................................................................................................

4. Kazi yako
    a) Mwanafunzi
    b) Umeajiriwa

c) Umestaafu

d) Mfanyibiashara

e) Mwalimu

f) Mwandishi wa habari

g) Nyingineyo bainisha...........................................................................................

5. Uwezo wako wa kuzungumza Sheng.

a) Mzuri sana

b) Mzuri

c) Kiasi

d) Mbaya

**Sehemu b**

1.Je, Sheng kama lugha ina maendeleo yoyote ya kimsamiati na kisemantiki?

a) Ndio

b) La

2.Maendeleo hayo yanaweza kujitokeza kama ubunifu wa kileksimu?

a) Ndio. Toa mifano ya leksimu mpya na maana zao au leksimu ilipata maana mpya.

...................................................................................................................................

...................................................................................................................................

b) La. Toa sababu...........................................................................................................

3.Je, Sheng ina uwezo wa kufanikisha mawasiliano miongoni mwa wazungumzaji?

a) ndio........................kwa nini?.......................................................................................

b) La.........................kwa nini?........................................................................................

4. Je, Sheng ina mfumo wowote wa kisemantiki?

a) ndio

b) la

5. Je, maana za maneno ya Sheng zinabadilikabadilika?

a) ndio....................toa sababu...........................................................................................

b) la.......................toa sababu............................................................................................

6. Je, huwa unatumia maneno kwa maana zao za zamani au maana mpya

a) ndio

a) la

mfano

| **neno** | **maana asilia** | **maana mpya** |
|---|---|---|
| manga | kula chakula | kufanya mapenzi |
| dunga | toboa | valia nguo |

7. Toa mifano zaidi ya maneno ya Sheng yaliyobadili maana zao

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

8. Je, Sheng hubuni msamiati mara kwa mara?

a) Ndio

b) la

i. Kama jibu lako la 8 ni ndio, toa mifano ya misamiati mpya na maana..........................................

..........................................................................................................................................

ii.Kuna wakati Sheng hubuni msamiati hata pale ambapo tayari kuna msamiati hivi kwamba kuna visawe vingi kama mifano hii; *fadhee- buda- mbuyu.*

iii.Toa sababu yoyote ya mfanyiko kama huo................................................

..........................................................................................................................................

9. Huku ukifuata mtindo wa neno la awali kabisa toa seti nyingine ya msamiati uliobuniwa.

   Kwa mfano; fadhe-buda- mbuyu

   a)........................................................................................................................

   b)........................................................................................................................

10 Kwa nini wazungumzaji Sheng hupendelea msamiati fulani fulani badala ya mwingine? Toa sababu..........................................................................................................................

..........................................................................................................................................

11. Mbona msamiati katika A zitumike badala ya B ilhali maana zao zinakaribiana.

| A | B |
|---|---|
| Buda | mbuyu |
| Manzi | chik |
| Ganji | chums |
| Masa | madhe |
| Mahewa | ngoma |
| Wezere | rasa |

i.Toa sababu zako..................................................................................................................

ii. Tumia nambari 1,2,3.........kuendelea kubainisha msamiati uliotumika mwanzo hadi ule unaopendelewa kwa sasa. K.m a) katia**1** hanya**2**

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| a) | Jamaa | chalii | | | |
| b) | Pai | karao | koopa | gava | |
| c) | Ushago | shake | shags | ocha | |
| d) | Chik | demu | kenge | manzi | mshii |
| e) | Ashara | ashu | kinde | | |

12. Je, msamiati wa Sheng hupoteza maana zozote? Kama ni ndio toa sababu..........................................

.......................................................................................................................................

i. Orodhesha mifano ya maneno yaliyopoteza maana zao, bainisha maana ya awali na ile mpya...................................................................................................................

.......................................................................................................................................

13. Je, msamiati wa Sheng hupata maana nyingine mpya? Kama ndio toa sababu................................

.......................................................................................................................................

i. Orodhesha mifano ya maneno yaliyopata nyongeza za maana, bainisha maana za awali na zile za nyongeza..........................................................................................................

.......................................................................................................................................

14. Kulingana na wewe, huku ukibainisha kama ni nomino au kitenzi nini maana za maneno yafuatayo?

a) Bamba.......................................................................................................................

b) Bonga.......................................................................................................................

c) Mahewa.....................................................................................................................

d) Ngoma.......................................................................................................................

e) Gava..................................................................................................................................

f) Karao..................................................................................................................

g) Dema...............................................................................................................

h) Ndai ......................................................................................................................

i) Buu..........................................................................................................................

j) Dinga.......................................................................................................................

k) Njeve.......................................................................................................................

l) Rasa.........................................................................................................................

m) wezere................................................................................................................

n) Tegea ......................................................................................................................

o) Sota.......................................................................................................................

p) Chuo.......................................................................................................................

q) Manga....................................................................................................................

r) Wahi....................................................................................................................

s) Hanya......................................................................................................................

t) Katia...........................................................................................................................

u) Nyoora....................................................................................................................

v) Sembe....................................................................................................................

w) Dara........................................................................................................................

**Ahsante sana kwa muda wako.**